

MAFUNZO JUU YA MUSA



Sawa. Mungu akubariki, Ndugu Neville. Habari za asubuhi, marafiki. Inabidi niangalie mara moja moja ili kujua kama ni asubuhi au jioni. Vema, nina furaha kuwa hapa asubuhi ya leo. Ni joto, na hakika mna makaribisho mazuri. Hatuna majira ya kuchipua tena; tuna majira ya kiangazi na baridi kali hapa, sivyo? Kila kitu kinaonekana kimeenda kombo, kwa njia fulani.

² Vema, kilichonichelewesha, ni—ninasafisha nyumba. Nami nilikuwa na mavune na kuumwa asubuhi ya leo. Na niliamka mapema sana, ila sikujua mwanamke alikuwa na kazi nyingi hivi za kufanya, inawabidi kuwatayarisha watoto watatu kisha waondoke kwenda shule ya Jumapili. Loo, jamani! Mengi sana ya kufanya, zaidi ya nilivyodhania yalikuwako kufanya. Ndipo nikawazia, “Vema, sasa...” Jana jioni nilikuwa ninafanya kazi, na—nami ni—nilitoka kwenye huduma ya kiinjilisti...?... Jamani, si ni vigumu kupata kazi? Hum! Nilitoa dola thelathini na tano kwa wiki kwa mtu kumtunza mtoto, na hakuna mtu angefanya hiyo.

³ Jamaa fulani aliandika makala kwenye gazeti hapa si muda mrefu uliopita. Bila shaka, hili haliendi kwa hii. Alisema alikuwa hapa juu, mwanasiasa wa namna fulani huku Kentucky, akasema alikuwa jeshini mara mbili, alikuwa amejeruhiwa mara tatu, kama shujaa, alikuwa ameishi raia kwenye ujirani huo, alikuwa amefanya mambo mengi, akayaokoa maisha ya watoto wawili, na mmoja kutoka kwenye kijito na mwingine kutoka kwenye kitu kingine, nasahau yote aliyolazimika kufanya. Basi hatimaye akawazia, vema, inawabidi kuweka ujirani sawa, angegombea kiti fulani. Basi alipofanya hivyo, kutoka kwa watu laki moja, alipata kura tano. Akamuuliza liwali kama angeweza kupata bunduki iliyokarabatiwa ili imsaidie kutoka katika ujirani huo, kasema, “Ilikuwa ni hatari hata kuishi humo mjini.” Hakuwa na marafiki wa kutosha wa kumsaidia kutoka mjini. Hiyo ndiyo shukrani ya Marekani, hata hivyo, sivyo? Hiyo ni kweli. Huku Marekani, kadiri unavyofanya mengi, ndivyo unavyotarajiwa kufanya zaidi. Hiyo ni kweli, mengi zaidi yanatarajiwa kutoka kwako.

⁴ Vema, ninataka kutoa pongezi zangu asubuhi ya leo kuhusu jinsi kanisa linavyoonekana safi na zuri. Na nilipokuwa nikipanda kuja huku, walikuwa na mlango pale wa kutoa mzunguko mzuri zaidi wa hewa. Kwa hivyo hiyo ni nzuri sana, yeyote ambaye yuko kwenye halmashauri ya wadhamini hapa na alisaidia kuanzisha hili. Hakika hiyo ilikuwa nzuri sana, na ni kazi nzuri safi. Nafikiri Ndugu Hall, kama sijakosea, alifanya hivyo. Hiyo ni kazi nzuri sana.

⁵ Sasa, kumechelewa kidogo, lakini mnajua jinsi watu wa utakatifu walivyo. Unaona, hatuna wakati maalum, sivyo, Ndugu Slaughter, Ndugu Deitsman? [Ndugu hao na wengine wanasema, “Hakuna.”—Mh.] Kila kitu tu kama tunavyokichukua.

⁶ Tulikuwa na mikutano mizuri sana huko Kusini! Lakini ningeweza tu kuzungumza siku chache zilizopita. Nilihubiri kwa muda wa miezi minne, moja kwa moja, na sikuwa na sauti ya kutosha hata—hata kunong’oneza. Ilinibidi tu kumwashiria mke wangu, mwajua, nilichotaka, na kidogo ni... Kisha baada ya hayo, na kurudi huku juu ambako kidogo kuna baadhi ya hali hii ya hewa ya kinafiki tumekuwa nayo, (mbona, baridi siku moja na joto kesho yake), nikashikwa na mafua kweli kweli, ya mtindo wa kale. Ndipo nikaamka, siku chache zilizopita, na kuanza tena. Na kwa hivyo tunamshukuru Bwana mwema, hata hivyo, kwa wema Wake wote na rehema Zake kwetu, na—na jinsi ambavyo amekuwa mwema. Tulikuwa na mikutano mizuri sana huko chini, na Bwana akatubariki sana, kwa wingi.

⁷ Kisha jana usiku, karibu na usiku wa manane, Ndugu Wood aliniita nyumbani kwake, na Ndugu Arganbright kwenye simu, akitaka nianzie Uswisi. Kwa hiyo, ni mengi sana yanayotendeka kwa mzee.

⁸ Kwa hiyo, sasa, mkutano wetu unaofuata unaanza tarehe kumi na moja ya mwezi huu ujao, kwenye Maskani ya Cadle huko Indianapolis. Kwenye—kwenye Maskani ya Cadle huko Indianapolis, kuanzia tarehe kumi na moja hadi kumi na tano. Na kisha, kutoka hapo, hadi—hadi Minnea... Minneapolis; kutoka Indianapolis hadi Minneapolis, Wafanyabiashara Wakristo.

⁹ Sasa nafikiri Ndugu Neville alinipigia simu, nami nilitaka kuonyesha ninii yangu... kutoa shukrani zangu kwake na wale waimbaji watatu wa Neville walioshuka na kuniambia kwenye yale mazishi, niliyokuwa nayo hivi majuzi. Nami nilimwuliza Ndugu Neville; sikuwa na waimbaji wowote, familia ya Liddick; wakati Bw. Liddick alipokuwa ameenda Nyumbani Utukufuni. Nami hakika... ikiwa mwanawe, simwoni hapa; nami niligundua baadaye alikuwa ni mwana wa kulea. Akijua babake alikuwa yuafa, hajaokoka, alikimbia nyumbani kunichukua, kabla yeye... ndipo baba yake akaokoka kabla hajafa. Kwa hiyo jambo kuu sana ambalo mvulana huyo aliwahi kufanya, lilikuwa ni kuja kumchukua mtu wa kumwomba baba yake kabla ya kuondoka. Nao wale waimbaji watatu wa Neville wakashuka na kuwambia nyimbo za kupendeza sana.

¹⁰ Na kwa hiyo Ndugu Neville akaniomba kama ngingezungumza asubuhi ya leo na jioni ya leo, pia. Kwa hiyo unaona, Maandiko yanasema, “Ombeni kwa wingi ili mninii...”

Kwa hiyo Ndugu Neville hakika ni wa Kimaandiko juu ya mambo hayo, sana! Na kwa hivyo nitafanya vizuri niwezavyo.

¹¹ Sasa, nilisema asubuhi ya leo, kwa kuwa ni Siku ya Mama, basi tunataka kuzungumza na—na watoto wadogo. Nilifikiria asubuhi hii itakuwa ni wakati mzuri kwa—kwa watoto wadogo. Sasa nafikiri kwamba siku ya mama . . .

¹² Sasa, hakuna chochote kinachopendeza zaidi duniani, tukijuacho, kuliko mama halisi, wa kweli. Mungu aibariki nafsi yake shujaa, mama halisi, halisi kabisa. Lakini tuna vibadala vingi sana siku hizi vi—vinavyoitwa “mama,” ambavyo si mama; wao ni wanawake tu ambao wana watoto, lakini si mama. Mama wa mtindo wa kale ni yule anayeishughulikia familia yake, wala hatangatangi kwenye vyumba hivi vya anasa na madansi, na usiku kucha, akivuta sigara, akinywa pombe, kuingia. Hastahili jina hilo takatifu la mama. Yeye ni mwanamke tu, hivyo tu, anayemlea mtoto; lakini si mama, maana *mama* lina maana tofauti. Sasa na—nadhani ikiwa wewe . . .

¹³ Sasa, kwa Siku ya Mama, ninataka kujieleza vizuri sana. Nina mama mzee mwenye mvi ameketi pale, mimi mwenyewe. Nami nafikiri, siku moja, vema; lakini kila siku inapaswa kuwa siku ya mama, si mara moja tu kwa mwaka. Na sababu ya mambo haya ya Siku ya Mama kuendelea sasa . . .

¹⁴ Nami naona tuna wachache tu, na sote tunafahamiana. Sisi ni jamaa wa nyumbani, na hiyo ndiyo sababu tunaenda kuzungumza hivi.

¹⁵ Nafikiri kwamba mama anapaswa kuheshimiwa kila siku vivyo hivyo, hiyo ni kweli, mama halisi. Na, lakini siku hii wanayoiita Siku ya Mama, si kitu ulimwenguni ila ni upuuzi mkubwa wa kibiashara, wapate tu kuwamalizia watu pesa. Na ni fedheha kwa mama, Siku ya Mama, mara moja kwa mwaka, “Vema, hatuendi kumwona, lakini tutamtumia shada dogo la maua na hilo litatosha.” Huyu sio mama! Jamani, masalale! Mama halisi ni mwanamke ambaye wewe . . . yule aliyekulea, nawe unampenda, nawe unamwona na kuzungumza naye wakati wote. Unamwonyesha upendo wako kwake wakati wote, sio siku moja tu katika mwaka.

¹⁶ Lakini kabla tu sijaanza maskini mchezo wangu wa kuigiza, ningependa tu kueleza hili, na kufanya upya . . . Baadhi yenu, wengi wenu wamekufa, wengi wao wametuaacha tangu huu ulipotolewa. Ilikuwa mwaka wa 1933.

¹⁷ Je, mliona kwenye gazeti siku chache zilizopita usiku ambapo yule mwanamke alimuua yule mwanamume? akamrusha nje kwenye njia ya kuingia nyumbani kwake na kumkanyaga-kanyaga kwa gari lake mpaka akamponda-ponda kabisa barabarani. Nao wakasema, ma—mawakili na kadhalika, wakasema, “Hivi hilo hali hukumu dhamiri yako?”

Akasema, “Mimi pamoja na Mungu tunachoka na jinsi wanawake wanavyotendewa.” Huh! Naam, yeye ni kijimungu. Hilo ni sawa. “Tunachoshwa.” Taifa hili linaweza kushuka chini kiasi gani? Tunaweza kwenda umbali gani bila hukumu ya Kiungu, nashangaa? “Mimi pamoja na Mungu”? Kama Mungu angalikuwa na hatia ya upuuzi wote anaowekelewa, hangekuwa Mungu, hivyo tu. “Mimi pamoja na Mungu”? Jamani! Mungu hahusiki na kitu kama hicho. Sijui atakapokuwa huko ng’ambo katika mateso, jinsi atakavyoliwazia basi? Loo!

¹⁸ Marekani! Sasa kumbukeni, kama hujaliandika hili, liandike. Huu ni ubashiri wangu. Mnaona? Mnamo 1933, tulipokuwa tukifanya ibada hapa chini ambapo lile la kale, ninaamini Church of Christ liko pale sasa, lilikuwa ni lile la kale. . . Liko papa hapa, Ndugu Neville, moja kwa moja kule chini. Charlie Kern alikuwa akiishi huko. Kile ilicho. . . Nyumba ya watoto yatima hapa kwenye Barabara Kuu ya Meigs. Mnamo 1933, nilikuwa tu nimenunua Ford ya 1933, na nikaiweka wakfu asubuhi hiyo kwa Bwana. Na, kabla ya kuondoka nyumbani, niliona ono. Nimeliandika, karatasi kuukuu ya manjano ingali kwenye Biblia. Niliona wakati wa mwisho ukija.

¹⁹ Na, ninyi, ni wangapi wanaoweza kukumbuka jinsi gari la ’33 lilivyoonekana huko nyuma? Loo, lilikuwa limevutwa namna *hii*, na huko nyuma juu kabisa, na kukatwa ili tairi la akiba lining’inie. Niliona ono, kwamba, “Kabla ya Kuja kwa Bwana, kwamba magari yangepanana na yai.” Ni wangapi wanaokumbuka ubashiri huo? Je, kuna mtu yeyote aliyesalia humu? Ndugu Seward ameondoka. Nami nadhani. . . Ilikuwa 1933 tulipokuwa tukifanya ibada hapa. Nadhani karibu wote wametuaacha sasa, tangu wakati huo.

²⁰ Kisha nikabashiri, kwamba, “Marekani, mungu wao wa kwanza angekuwa ni wanawake.” Ndivyo ilivyo. Kila kitu kina muundo wa Hollywood. Nina mambo kwenye kumbukumbu kutoka kwa faili ya FBI ambayo yanaweza kukushtua kabisa ku—kuwaambia tu, mahali hasa. . . Na kashfa juu ya hawa nyota wa filamu, hakuna hata mmoja wao, angalau, ila ni makahaba. Nayo FBI ililifichua hilo hivi majuzi tu. Ninayo kutoka kwenye faili yao wenyewe. Na kwa hiyo wote wakiishi huko nje, hata hawa nyota wa filamu, ambapo alithibitisha, waliingia na kuwachukua, wakiishi na wanaume, dola ishirini na tano na hamsini kwa usiku mmoja, mwanamume, kote huku na huku, huko Hollywood na kila mahali, walikuwa na nyumba za kibinafsi na wanaume huko nyuma ambako wangewatuma kwa watu hawa. Na hao ndio tunaowaangalia, televisheni, na—na hapa nje kwenye skrini hizi na kadhalika, na kuwaacha watoto wetu wawaite hao kijimungu. Halafu ati huyo aitwe *mama*? Hao wako mbali sana na kuwa mama. Huo ni uchafu. Hiyo ni hakika. Na hata hivyo wanaweka mtindo wa kisasa. Tunawaruhusu. . . aina ya mavazi

wanayovaa, tunawaona wanawake wa Kimarekani wakivalia kama wao kabisa, na kila kitu. Hakika. Basi mungu wa Marekani ni mwanamke. Si Yehova; wamemwacha Huyo. Si kwa *mama* sasa, sasa mweke huyo kando, hilo ni jambo takatifu tutakalozungumzia; lakini namaanisha *mwanamke*.

²¹ Pia, kumbukeni, ninabashiri ya kwamba kabla ya yale maangamizi makubwa kabisa, ambayo sisemi Bwana aliniambia hili, lakini naamini kutakuwa na kitu kitakachotokea kati ya sasa au wakati huo katika mwaka wa '77. Kinaweza kutokea kwenye saa hii. Lakini kati ya sasa na '77, Ninabashiri kwamba ama uharibifu mkubwa au maangamizi kamili ya dunia nzima, kati ya sasa na '77.

²² Nililibashiri, mnamo 1933, nilibashiri kuwa wanawake wataendelea kukosa maadili na taifa litaendelea kuanguka, nao wangeendelea kuning'inia kwa mama, ama kama mama namna hiyo, mpaka wawe, mwanamke awe kijimungu. Na baada ya muda kidogo, kwamba, "Marekani ingetawaliwa na mwanamke." Lishikeni hilo muone kama si kweli. Mwanamke atachukua mahali pa Rais ama kitu fulani, mamlaka fulani makuu, Marekani.

²³ Ambapo, nasema hivi kwa heshima, enyi kina mama, mwanamke anapotoka jikoni, yuko nje ya mahali pake. Hiyo ni kweli. Hapo ndipo mahali pake. Nje ya hapo, yeye hana mahali. Na sasa, mimi siwakandamizi, bali ninasema tu kile ambacho ni Kweli na kile ambacho Biblia... Zamani mwanamume ndiye aliyekuwa kiongozi wa nyumba, lakini hiyo ilikuwa katika siku za Biblia. Yeye siye tena. Yeye ni kibaraka, au yeye ni... au yaya ama chochote kile. Na sasa, hapana, wanataka kuhudumia mbwa, kupanga uzazi, na kubeba maskini mbwa wa kale mikononi mwao wakati wote, ili uweze kuzurura usiku kucha.

²⁴ Si—sizungumzi juu ya mama. Mungu awabariki. Huyo ndiye anayelishikilia taifa pamoja sasa, nusu, ni mama halisi, mzuri, mtakatifu, aliyeokolewa na Mungu. Hiyo ni kweli.

²⁵ Lakini ni aibu jinsi wanawake wetu walivyojidhalilisha! Nina kijipande kutoka gazetini, nilikikata baada ya Vita hivi vya mwisho vya Dunia, namba mbili, kilichosema, "Maadili ya wanawake wa Marekani yameenda wapi, hivi kwamba, baada ya miezi sita nje ya nchi, askari wanne kati ya watano walitalikiwa na wake zao, nao walikuwa wameolewa na wanaume wengine?" Wala wasingeweza hata kuwangojea warudi kutoka nchi za ng'ambo, askari kule wakifa kwenye uwanja wa vita! Mtu huyo anayefanya hivyo hastahili kuitwa mama, jina hilo takatifu. Hapana, sivyo. Kwa hivyo sikuzote nimeitwa "mchukia wanawake," lakini sivyo nilivyo. Nafikiri mwanamke ni kitu cha ajabu, na mama, hasa. Lakini wanapaswa kukaa mahali pao wala si kuchukua mahali pa mwanamume, na wasipachukue mahali pa Mungu.

26 Na asubuhi ya leo nilisikia kanisa la utakatifu likisema, ya kwamba, “Mama hutawala nyota za Mbinguni,” na haya yote. Ninaweza kuwawazia Wakatoliki wakifanya hivyo kwa bikira Mariamu, na kadhalika namna hiyo, ambao, wanawaabudu hao wanawake waliokufa, Mtakatifu Sisilia na wote namna hiyo, ambao ndiyo hali ya juu kabisa ya uabudu mizimu. Hivyo ndivyo tu yalivyo. Chochote kinachoshirikisha wafu katika maombi ni uabudu mizimu. Kwa hiyo, kuna Mwombezi mmoja tu kati ya Mungu na mwanadamu, na huyo ni Kristo Yesu. Hiyo ni kweli. Hakuna mtakatifu mwingine, hakuna chochote nje ya Bwana Yesu Kristo Ndiye Pkee aliye Mwombezi kati ya Mungu na mwanadamu. Lakini ninapoyaona makanisa, hata na kwenda nyuma ya mimbara, utakatifu wote umetolewa kwa Kristo na kupewa mama, utakatifu wote umeondolewa, basi—basi wanaanza na hakuna lingine.

27 Kwa hiyo, lakini kuna mama halisi aliyesalia. Mungu asifiwe! Kama vile tu ukimwona mnafiki; kuna Mkristo halisi ambaye kweli anayaishi hayo maisha. Unapokuwa na ubaya, una uzuri. Hiyo ni kweli kabisa. Na sasa, mama wa namna hiyo na mtoto wa namna hiyo, ndio tunaotaka kuzungumza habari zao sasa katika Biblia.

28 Sasa nashangaa, ni wavulana na wasichana wangapi tulio nao hapa asubuhi ya leo? Kama ulisikia matangazo ya Ndugu Neville jana... Ni wavulana na wasichana wangapi wadogo wangependa kuja hapa na kuketi kwenye kiti cha mbele ninapozungumza nanyi? Je, mngependa kuja hapa juu? Kuna viti moja, mbili, tatu, nne, tano hapa; moja hapa, ni sita, na baadhi ya viti vidogo hapa. Je, mngependa kusonga mbele, baadhi yenu nyinyi watoto wadogo mnaoweza kwenda bila mama zenu, na mngependa kuja hapa juu? Mmekaribishwa hata na zaidi! Akina mama njoni... [Ndugu Neville anasema, “Kuna wengine; wengi wao katika chumba cha shule ya Jumapili.”—Mh.] Loo, wako kwenye chumba cha shule ya Jumapili. Vema, hiyo ni sawa. Tutasubiri dakika chache, na tuendeleo kuzungumza, nao watatoka baada ya dakika chache. Nasi tutawakusanya tu, macho madogo meusi, na kahawia, na ya samawati, hapa juu, na—na kuzungumza na kila mmoja wao. Sasa, ni wangapi wanaompenda Bwana? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina!”] Vema.

29 Sasa nataka kuzungumza na akina mama na watoto, na limeelekezwa kwao.

30 Usiku wa leo, Bwana akipenda, nataka kuzungumza juu ya muujiza wa kwanza aliofanya Yesu, na jinsi ulivyofanyika, na kwa nguvu gani, Naye alifanya nini alipoufanya ninii Wake... Ni wangapi wanaojua ule muujiza wa kwanza aliofanya? Semeni, nyote pamoja: “Aligeuza maji kuwa divai.” Hiyo ni kweli, muujiza wa kwanza aliofanya. Sasa, Bwana akipenda.

Nilipokuwa nikisoma, asubuhi ya leo, lilinijia tu akilini mwangu.

³¹ Ninaona tuna rafiki yetu mwema, Bw. na Bibi Yeker kule nyuma, naamini, asubuhi ya leo. Ilitokea tu niliwaona nilipogeuka kuzunguka nguzo hii hivi. Hivi majuzi nilifanyiwa uchunguzi; sina budi kujiandaa kwa ajili ya uchunguzi kuhusu huduma za nchi za ng'ambo. Na, nilipotoka nje, nilikutana na nani ila Bw. na Bibi Yeker, wameketi huko nje ofisini—ofisini.

³² Dk. Schoen, huko Louisville, ndugu Mkristo mzuri sana. Nawaambia, kweli nilikutana na mtu halisi huko, mtu halisi aliyemwamini Mungu na anaweka tumaini lake hapo. Mnajua nini? Nitawaambia. Ninakuta madaktari wengi zaidi wanaoamini katika uponyaji wa Kiungu kuliko ninavyokuta wahubiri. Hiyo ni kweli. Hebu zungumza nao. Kasema, "Hakika." Na wakati yeye... Nilipoanza kutoka, aliushika mkono wangu, akasema, "Ndugu Branham, unafanya mengi zaidi kwa ajili ya wanadamu kuliko ningaliweza kufanya." Akasema, "Hiyo ni kweli." Kasema, "Unaweza kuwasaidia watu ambao hata nisingeweza kuwagusa." Kasema, "Hiyo ni kweli."

³³ Nikasema, "Vema, bila shaka, unaweza kushona, ama kurudisha mfupa, ama kitu kama hicho. Lakini Mungu huponya."

³⁴ Akasema, "Hiyo ni kweli." Amina. Loo, napenda kuona watu wenye nia pana, wenye akili timamu. Ninawazia juu ya upasuaji, na juu ya daktari wa tiba, na juu ya tabibu wa viungo, tabibu wa mifupa, uponyaji wa Kiungu, na wote kwa jumla, kama yeyote kati ya hao anaweza kumsaidia mtu yeyote, naliunga mkono. Basi unapomwona daktari akimhukumu mhubiri; mhubiri akimhukumu daktari; na tabibu wa mifupa akimhukumu—akimhukumu daktari wa upasuaji; daktari wa upasuaji akimhukumu daktari wa tiba; unaweza kuwazia hili, kuna nia ya ubinafsi mahali fulani. Hiyo ni kweli, maana kila mmoja wao amethibitisha ya kwamba wanamsaidia mtu fulani. Hiyo ni kweli kabisa.

³⁵ Sasa jambo ni kwamba, nafikiri, kama nia zetu ni sawa, na mioyo yetu ni sawa kwa watu, sote tunapaswa kufanya kazi pamoja kuwasaidia wanadamu wenzetu, kuyarahisisha maisha. Ndipo basi nia zako hazina ubinafsi, ukimpa Mungu sifa ambaye hutoa kila kitu bure. Amina. Naam, bwana. Loo, hatupaswi kuwa na ubinafsi wowote mahali popote; inapaswa kuwa kikamilifu.

³⁶ Ikiwa tabibu wa viungo anaweza kumsaidia *huyu*, na tabibu wa mifupa amsaidie *huyu*, tabibu wa upasuaji amsaidie *huyu*, na kitu kingine kimsaidie *yule*, na tuwaombee hao wote, amina, kwamba Mungu atawasaidia tu watu Wake wapendwa kuwa wazima na wenye furaha. Maana, hatuna muda mrefu sana wa

kuishi hapa, siku chache tu nasi tuko njiani, tumeenda mahali pengine. Kwa hivyo tunachojaribu kufanya ni kurahisisha maisha ili uwe na wakati mzuri zaidi wakati ukiwa hapa. Amina.

³⁷ Sasa juu ya wazo hili, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kabla hatujaifungua Biblia, na kuzungumza na Mwokozi wetu mpendwa.

³⁸ Baba yetu wa Mbinguni mwenye fadhili, tunakuja kwa unyenyekevu sana asubuhi ya leo katika Uwepo Wako, na kukushukuru Wewe zaidi ya kila kitu kilichowahi kuwako duniani, ama kitakachopata kuwako, kwa ajili ya Bwana Yesu Kristo. Kwa maana, Yeye alikuwa Ndiye Yule aliyeleta pamoja mwanadamu na Mungu, na kutupatanisha sisi maskini tusiostahili, wageni waovu, mbali na Mungu, kwa—kwa hiari, yetu wenyewe, tulijichagulia wenyewe na kumwacha Yeye. Naye alikuwa mwema sana kuja, na wakati tulipokuwa hatumpendezi Mungu, tulipokuwa wenye dhambi, mbali na Mungu, alitupatanisha tena na Baba, kupitia kwa kumwagwa kwa Damu Yake Mwenyewe.

³⁹ Jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili Yake! Na leo hii amesimama kama Mpatanishi, wa pekee kati ya Mungu na mwanadamu, Yeye awezaye kufanya maombi yaje Mbele za Mungu, kupitia jukwaa la Damu Yake Mwenyewe aliyomwaga kutoka duniani hata Utukufuni. Akaja humu duniani kwa njia ya zizi, akazaliwa katika hori. Akatoka duniani, kupitia adhabu ya kifo. Dunia haikumtaka. Mbingu hazingeweza kumpokea, kwa sababu alikuwa mwenye dhambi, alikuwa amejitwika dhambi zetu. Dunia haikumtaka. Walimkataa, “Jiepusheni na Mtu kama huyo!” Alikuwa na hata...hana hata mahali pa kuzaliwa, wala mahali pa kufia. Naye akaning'inizwa kati ya Mbingu na nchi; Mbingu hazingeweza kumpokea, wala dunia isingemkubali. Naye alikufa, hata hivyo, apate kutuokoa na dhambi, kuponya maradhi yetu, kutupa furaha na ukaaji mzuri wakati tukiwa hapa duniani. Ni Mwokozi wa jinsi gani! Loo, jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili Yake!

⁴⁰ Ee Mungu, acha kila ibada ya mioyo yetu imwagwe Kwake, na Yeye pekee. Jalia kila heshima na kila ibada, kila kitu kinachotoka kwenye midomo au mioyo yetu, jalia kiwekwe juu Yake Yeye anayestahili yote, Yeye aliyeketi juu ya Kiti cha Enzi siku moja, ameshika Kitabu mkononi Mwake. Hakuna mtu Mbinguni wala duniani aliyestahili ama kuweza hata kukitazama kile Kitabu, ama kuifungua ile Mihuri iliyokuwa imekitia muhuri. Naye Mwana-Kondoo huyu aliyekuwa amechinjwa, msingi wa dunia, akaja, akakitwaa kutoka mkononi Mwake, akaifunua ile Mihuri na kuyafungua ha—hayo Maneno, kwa watu.

41 Na, Baba, tunaomba leo kwamba Roho Wake Mtakatifu ataifungua mioyo yetu kutoka katika giza lake lote, kuufungua ulimi wetu kutoka kwa yote yaliyo maovu, atusamehe dhambi zetu zote, na kuondoa giza lote, na kuingia ndani ya mioyo yetu asubuhi ya leo.

42 Na hasa sana watoto hawa wadogo, Mungu, wabariki wanapoketi hapa asubuhi ya leo pamoja na mama yao mpendwa. Mungu, jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya umama, kwa ajili ya wanawake halisi! Katikati ya giza hili lote na uabudu sanamu, na uchafu na ufisadi wa ulimwengu, hata hivyo tunao mama halisi, wa kweli. Jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili yao! Vijana kwa wazee, wote sawa, tunakushukuru Wewe, Baba, kwa ajili ya umama halisi. Nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba utawabariki.

43 Tukiona, wengi wa ndugu na dada zetu walioketi hapa asubuhi ya leo wamevaa waridi nyeupe au karafu nyeupe na maua, ikimaanisha kwamba mama yao mpendwa mtakatifu amevuka ng'ambo ya pazia, ng'ambo ya pili; hajafa, bali yu hai hata milele. Siku moja watakuja, pia, huko chini mtoni, na huko watamwona tena, upande ule mwingine. Wengi wamevaa waridi nyekundu, mama bado yuko hapa. Tunakushukuru kwa hilo.

44 Tunaomba kwamba utatubariki pamoja tunapojifunza Neno Lako, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Kristo. Amina.

45 Sasa Bwana awabariki. Nasi tunaanza moja kwa moja kwenye Neno asubuhi ya leo. Sasa, kwanza, kabla ya mchezo huu mdogo wa kuigiza, niliwazia akina mama na watoto wadogo... Na labda watanisikia, kwa maana kitu hiki kina sauti kubwa kweli. Na nittoa mchezo mdogo wa kuigiza, kwa sababu nimekuwa nikiona sasa ibada zangu, wakati mwingine michezo ya kuigiza husaidia sana. Hamfikirii hivyo? Hawa jamaa wadogo wanaelewa huo vizuri zaidi. Ninatazama baadhi ya wavulana wadogo, wenye macho maangavu wameketi, wakinitazama sasa, ambao watakuwa wanaume wa kesho endapo kuna kesho.

46 Na sasa kabla hatujawa na mchezo wowote wa kuigiza, ama chochote kile kinachoendelea kanisani, hakina budi kuwa na msingi wa Biblia. Amina. Ni lazima uwe ni msingi wa Biblia. Kwanza, na tufungue sote kwenye Mathayo, mlango wa 16 na kifungu cha 25, nasi tutasoma vifungu hivi. Kwanza, tunaposoma, tukijitayarisha, labda kufikia wakati huo hao jamaa wadogo watakuwa wametoka. Sasa Mathayo 16:25, tunasoma hivi:

Kwa maana mtu atakaye kuiokoa nafsi yake, ataipoteza, na mtu atakayepoteza nafsi yake kwa ajili yangu, ataiona.

47 Sasa, haya ni Maandiko muhimu sana. Hebu sote tuyasome hayo pamoja. Mwasemaje? Kila mtu, watoto wadogo na

wote, pamoja sasa. [Ndugu Branham na kusanyiko wanasoma Maandiko yafuatayo pamoja—Mh.]

Kwa maana mtu atakaye kuiokoa nafsi yake, ataipoteza, na mtu atakayepoteza nafsi yake kwa ajili yangu, ataiona.

⁴⁸ Mnajua, enyi wavulana na wasichana, nami ninajua watu wazima watafurahia hili sawasawa na watoto watakavyolifurahia. Lakini, Maandiko hayo ni muhimu sana! Na Maandiko mengine ni muhimu sana hata Mungu anayaweka katika Injili zote nne: Mathayo, Marko, Luka, na Yohana. Lakini, hili lilikuwa muhimu sana mpaka akaliweka mara sita katika Injili! Mara sita haya yalitoka midomoni Mwake Mwenyewe, Yesu.

⁴⁹ Sasa katika Marko, tutafungua mle, kwenye mlango wa 8 wa Marko, na kuanzia na kifungu cha 34, nami nitasoma baadhi yake hapo. Nami nawatakeni muone hapa tena, kwa mwendelezo mdogo tu wa hili ambapo Yesu alilineni. Pia kumbukeni, Yeye aliyaweka mara sita katika Injili, ili yahakikishwe! Wawili ni shahidi, lakini Yeye aliyaweka mara tatu ya hayo, mnaona, kusudi ihakikishwe kwamba unayakumbuka.

A—akawaita mkutano pamoja na wanafunzi wake, akawaambia, Mtu yeyote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, . . . ajitwike msalaba wake, anifuata.

⁵⁰ Sasa, mmoja wa watafsiri aliyaweka, “Ajitwike msalaba wake anifuata kila siku.” Sasa, sasa kifungu cha 35. Sikilizeni:

Kwa maana mtu atakaye kuiponya nafsi yake, ataiangamiza; na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya injili, huyo ataisalimisha.

Kwa kuwa itamfaidia mtu nini kuupata ulimwengu wote, akipata hasara ya nafsi yake?

Ama mtu atoe nini badala ya nafsi yake?

⁵¹ Sasa hebu na tuchukue kifungu hiki cha 35 na tukinukuu pamoja sasa. Vema. Sasa hebu tuseme pamoja. Tutachukua Marko 8:16, sasa hebu tuseme pamoja; Marko 8:16, kunradhi, Marko 8:16, 35. La, bado nimekosea. Marko 8, samahani. Marko, Marko Mtakatifu, mlango wa 8, kifungu cha 35. Sasa hebu tujaribu. Marko Mtakatifu, mlango wa 8, kifungu cha 35. Sasa tumeipata. Hebu tuisome. [Ndugu Branham na kusanyiko wanasoma Maandiko yafuatayo pamoja—Mh.]

Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake, ataiangamiza; ila mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya injili. . . ataisalimisha.

⁵² Ajabu hiyo? Sasa, tutaendelea moja kwa moja na hadithi yetu ndogo, nao watoto wanapokuja watachukua mahali pao. Mabawabu wawaangalie wanaponinii, kwa unyamavu . . . muone kama mnaweza kuwaingiza humu, tunapochukua na kutoa

hadithi yetu. Tutawekea hili msingi, asubuhi ya leo, kwenye mchezo wa kuigiza. Nami, muda mwingi, hapa siku chache zilizopita mimi. . .

⁵³ Ndugu na Dada Wood walikuwa pamoja nami, naamini, huko juu kwenye mkutano uliopita, nami nilikuwa nikizungumza kwenye Kiamshakinywa cha Wafanyabiashara Wakristo. Nami nikatoa mchezo mdogo wa kuigiza juu ya Zakayo katika. . . juu ya mkuyu, ndipo, Yesu alipopitia pale, na jinsi alivyobeba pipa la takataka, mnajua (na kuigiza hilo), kisha akapanda juu ya mti, kumwona Yesu; huyo mfanyabiashara akiketi juu ya mti, mwajua, akijificha kutoka kwa Yesu. Naye Yesu hakujua alikokuwa, kana kwamba, mwajua. Kisha akasema, “Loo, wananiambia kuwa yule Mtu anajua mambo na anaweza kutabiri mambo, na anajua mahali ambapo samaki alikuwa na sarafu. Siamini hilo.” Ndipo Yesu akaenda moja kwa moja chini ya huo mti. Naye akasema, “Loo, hawezi kuniona, nimeketi juu ya mti.”

⁵⁴ Yesu akasimama akatazama juu, na akasema, “Zakayo, shuka.” Hakujua tu kwamba alikuwa kule juu, bali alijua yeye alikuwa ni nani.

⁵⁵ Kwa hivyo nadhani mchezo mdogo wa kuigiza wakati mwingine huwasaidia wazee, wavulana na wasichana wakubwa, sawasawa na vijana.

⁵⁶ Kwa hivyo sasa mnaweza kuniuliza, baada ya hii kumalizika, “Ndugu Branham, unapata wapi habari hizi za wahusika hawa na majina?” Baadhi yao, nimesaidiwa na rafiki yangu mwema, Ndugu Booth-Clibborn. Na mwingine, na Josephus, yule mwanahistoria mashuhuri. Na halafu vitabu vya historia ambavyo nimesoma, vya tukio hili, na kadhalika. Na hivyo ndivyo ninavyopata habari zangu kutoka kwa kile tutakachotoa katika mchezo wa kuigiza asubuhi ya leo, kwa ajili ya hili.

⁵⁷ Ninaona watoto wetu wanatoka sasa, na kwa ajili ya hadithi hii asubuhi ya leo ambayo tutasimulia. Sasa ninyi wavulana na wasichana wadogo, mkiweza, wote wanaotaka, njoni moja kwa moja hapa mbele. Tuna viti vitano au sita vitupu. Ikiwa mngependa kuja moja kwa moja huku juu, tutafurahi kuwa nanyi. Wanaingia tu kwa wakati mzuri wa mchezo mdogo wa kuigiza hapa.

⁵⁸ Na sasa hivyo ndivyo ninavyopata habari hii, jinsi ninavyoipata. Mtu anaweza kukosoa na kusema, “Vema, sikuwahi kusoma sehemu hiyo katika Biblia.” Lakini, kama hukusoma, historia iliichukua, unaona. Kwa hivyo yote ni hadithi ile ile, ila imetolewa tu katika m—m—mfano wa mchezo mdogo wa kuigiza.

⁵⁹ Na, hivyo, jambo ndilo hilo! Ndilo hilo! Huyu ni kakako mdogo? Loo, hakika anafanana na wewe! Naye ni mvulana mzuri. Unaweza tu kujua ni mzuri. Vema.

⁶⁰ Sasa unataka kuja hapa na kuketi hapa chini? Kuna wasichana wawili wadogo, au wasichana wadogo watatu. Jamani, hilo ni sawa na linapendeza! Sasa nataka... Hadithi hii ndogo asubuhi ya leo ni kwa ajili ya wasichana wadogo na wavulana. Binti Collins, ninaamini huyo ni wewe hapo, na yule dada mdogo mwingine; unataka kwenda pale pale, mpenzi, na kuketi. Naam, naamini kuna mahali papa hapa, kama mama huyo ange—angesogeza kitabu chake cha mfukoni. Na—na kisha papa *hapa* pana viti kadhaa hapa.

⁶¹ Nawataka hawa wavulana na wasichana wadogo wote hapa mbele, ili niweze kuzungumza nao. Hapa, hapa tuna viti hapa. Tunahakikisha tu kwamba mnapata viti. Naam, bwana. Baadhi yao watatusaidia papa hapa. Kwa hiyo, tunataka hili liwe tu kwa ajili ya hawa wavulana na wasichana wadogo. Loo, jamani! Hilo si ni sawa? Sasa hilo ni... Ninaamini ingekubidi kupata vingine vichache, Ndugu Neville, ninaona wengine wachache wakishuka. Na sasa hilo ni sawa tu!

⁶² Ni akina mama wangapi walio hapa? Inua mkono wako. Loo, hilo ni zuri sana! Sasa, hilo ni sawa tu na linapendeza.

⁶³ Sasa ikiwa ninyi wasichana wadogo huko nyuma mnataka kuja hapa, njoni moja kwa moja, ikiwa una umri wa kutosha kumwacha mama. Naye mama anataka kukuleta hapa juu, vema, mwambie aje moja kwa moja. Ni kwa ajili ya mama, pia. Vema, sasa.

⁶⁴ Ninawaambia, enyi watoto, tumesoma aya moja tu hivi punde. Je, nyote mngependa kuinukuu pamoja nami? Je, nyote mngependa kunukuu kifungu hiki pamoja nami? Sasa, kinapatikana katika Mathayo Mtakatifu, mlango wa 16 na kifungu cha 25, kile ambacho tutazungumzia. Sasa maskini hawa... Kila mvulana na msichana mdogo, asubuhi ya leo, anukuu hili pamoja nami sasa: [Wavulana na wasichana wanarudia nyuma ya Ndugu Branham—Mh.] Semeni, “Mathayo Mtakatifu, mlango wa 16, kifungu cha 25.” Sasa nukuuni pamoja nami: “Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake, ataiangamiza; na mtu atakayeipoteza nafsi yake kwa ajili Yangu ataiokoa.” Ataiokoa. Hebu tuseme tena: “Mtu atakayeipoteza nafsi yake kwa ajili Yangu ataiokoa.” Ajabu!

⁶⁵ Sasa, enyi wavulana na wasichana, mnajua nini? Kuna vitu vingi ulimwenguni ambavyo ni vya thamani sana. Na moja ya vitu hivyo ni, unacho leo hii, ni nafsi iliyo ndani ya mwili huo. Na hicho ndicho kitu cha thamani zaidi duniani, kwako. Hiyo ni kweli, mama? Semeni, “Amina.” [Mama wanasema, “Amina.”—Mh.] Kitu cha thamani zaidi ulicho nacho ni nafsi yako. Na sasa ukiizuilia nafsi yako, basi utaipoteza. Na ukiipoteza nafsi yako, basi utaiokoa; ukipoteza nafsi yako kwa Yesu, unaona. Kwa maneno mengine, ukimwamini Yesu, unakuwa mwanafunzi Wake. Na basi ukimpa Yesu maisha yako ukiwa mchanga

hivi, ndipo basi utaninii... Yeye atayaokoa kwa Uzima wa milele. Lakini kama u—ukitaka kuyahifadhi, utayapoteza; naam, utapoteza. Ukitaka kutenda kama wasichana na wavulana hawa wengine hapa, na kwenda nje na kufanya kama wafanyavyo, basi uta—uta—utaiipoteza. Lakini kama unataka kuyatoa maisha yako kwa Yesu, basi utayaokoa kwa Umilele na daima.

⁶⁶ Sasa, kumbuka hilo sasa, kwamba ndicho kitu cha thamani zaidi ulimwenguni kote, ni maskini nafsi yako. Na ukiihifadhi, utaiangamiza; ukimpa Yesu, unaiokoa. Mnaweza kusema hilo pamoja nami? Kama... [Wavulana na wasichana wanarudia nyuma ya Ndugu Branham—Mh.] Semeni, “Nikiihifadhi, nitaipoteza; na nikimpa Yesu, nitaiokea.” Ni hayo tu! Sasa mumelipata. Hilo si ni... .

⁶⁷ Akina mama wote wanaofikiria hilo lilikuwa sawa, semeni, “Amina.” [Mama wanasema, “Amina!”—Mh.] Loo, hilo ni sawa! Hilo ni zuri.

⁶⁸ Sasa, mnaona, kuna jambo moja unaloweza kufanya. Sasa, endelea. Kama wakitaka kutenda hivyo, na kupata matakwa yao ya ulimwengu... . Kama wavulana na wasichana wanataka kwenda huko nje na kufanya vituko, na kusimulia hadithi na kusema mambo mabaya, na—na kudanganya na kuiba, na—na kufanya mambo mabaya, na kunakili shuleni, na kadhalika, waendele; wanapoteza. Wanaipoteza. Lakini kama utampa Yesu, hawatafanya hivyo, na kisha itaiokoa. Hicho ndicho unachotaka kufanya. Sivyo?

⁶⁹ Sasa tutaanza kwenye hadithi yetu ndogo. Sasa, huo ndio msingi wetu, sasa yakumbukeni hayo. Sasa hebu tuanze maskini hadithi yetu. Sasa, kwa wazee, na kwa a—akina baba na mama, sikilizeni, pia, sasa; ninyi, hasa ninyi akina mama na baba. Sasa tuninii tu... . na tutaanza. Mnapenda hadithi ndogondogo? Sivyo? Loo, ninazipenda sana! Hasa sasa... . Mnasoma hadithi nyingi ambazo si za kweli. Lakini hadithi hii ni ya kweli, Kweli kabisa, kila Neno lake. Iko katika Biblia ya Mungu, kwa hiyo haina budi kuwa Kweli, unaona, maana ni Neno la Mungu. Neno la Mungu ni Kweli.

⁷⁰ “Sasa, unajua,” kasema, “Nimechoka sana. Ni—ni—nimechoka nusura kufa.”

⁷¹ “Vema,” kasema, “kwa nini usiende ghorofani ukalale? Ulale kitandani, kwenye sofa huko juu, ukalale.”

⁷² Akasema, “Lakini, loo, nimechoka sana.” Akasema, “Loo, mpenzi, laiti ungaliona nilichoona leo! Loo, mimi ni... . mimi, kile... . Sitaki hata chakula chochote cha jioni! Loo, ni ya kuchukiza sana, tamasha nililoona leo!”

Kasema, “Vema, kwani uliona nini?”

⁷³ Kasema, “Kweli, siwezi kukuambia, mbele ya watoto, loo, ni la kuchukiza sana! Jamani, lilikuwa baya!”

“Vema, uliona nini?”

⁷⁴ “Vema, ninapanda ghorofani nilale kwa muda kidogo, na kisha—na kisha baada ya chakula cha jioni tutakapowalaza watoto wote kitandani, basi nitakwambia kilichotukia leo.”

“Sawa,” akasema.

⁷⁵ Huyu akapanda ghorofani. Akalala. “Loo, mchovu kweli! Loo, jamani!” Mnajua jinsi baba alivyo anapochoka, mchovu kwelikweli!

⁷⁶ Basi baada ya kitambo kidogo, maskini huyo msichana mwenye macho maangavu, akaanza kukimbia-kimbia sakafuni, na kuzungumza kwa sauti kubwa kidogo. Kasema, “Sh-sh-sh, sh-sh-sh, usifanye hivyo. Utamwamsha baba. Na, loo, amechoka sana hata a—alitaka kufa. Hakutaka kuishi tena. Na kama baba akichoka hivyo, vema, tunapaswa kumwacha alale kwa muda kidogo. Usimwamshe.” Basi mtoto Miriamu, anaenda huko na kuketi chini, ananyamaza kimya kabisa.

⁷⁷ Na baada ya muda kidogo akakiandaa chakula cha jioni, kwa hiyo akaingia polepole ghorofani na a—akamwita, “Amramu?”

⁷⁸ Naye akasema, “Naam, Yokebedi, mimi hapa. Nashuka.” Kwa hiyo wakashuka ngazi, mwajua, wakala chakula kizuri cha jioni.

⁷⁹ Basi wakiisha kula chakula cha jioni, basi yule mvulana m—mdogo na msichana mdogo wakiisha kula chakula chao cha jioni, mbona, wao . . . mama aliondoa vyombo na kuwalaza kitandani.

⁸⁰ Kisha anaingia chumbani, yeye na mumewe, wakaketi. Kasema, “Vema, sasa, uliona nini leo, Amramu, ambacho kimekufanya kufadhaika sa—sana usiku wa leo, hata hukutaka kuishi?”

⁸¹ “Loo,” akasema, “mpenzi, kamwe si—siwezi kulielewa.” Akasema, “Niliona . . . Vema, tunalionna kila siku, lakini leo lilizidi.” Kasema, “Loo, ni—niliona tamasha mbaya sana niliyowahi kuona.” Kasema, “Maskini wavulana wetu, baadhi yao wasiozidi umri wa miaka kumi na miwili, wakiuvuruta ule mkokoteni mkubwa wa kale, huku wamefungwa na kamba shingoni namna *hiyo*. Nao maskini hao watoto walikuwa wamevuta mpaka hawakuweza kuvuta tena, kwenye mwinuko huo mkubwa, hayo mawe makubwa kule nyuma, wala wasingeweza kwenda mbali zaidi. Ndipo baada ya kitambo kidogo huo mkokoteni ukaanza kukereza na kwenda polepole sana, na baadaye kidogo ukasimama. Huyu hapa mtu anashuka barabarani, loo, alikuwa mwendawazimu! Akawangurumia, ‘Mbona mnausimamisha mkokoteni huu?’ ‘Chwaa!’ kwa mijeledi hiyo mikubwa ya nyoka wa zamani, na kuwacharaza migongoni, na damu ikatiririka migongoni mwao, na kuteremka namna *hiyo*. Nao maskini watoto hao wakaning’inia tu kwenye kamba

hii na kulia.” Kasema, “Loo, Yokebedi! Tufanye nini, mama?” Kasema, “Sisi ni watu wa Mungu. Mungu alitubariki. Sisi ni watoto wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Na kwa nini itabidi tuwe watumwa hapa chini wa mambo haya? Loo, inatisha jinsi maskini wavulana hao walivyolia. Loo, na ninaomba na kuomba na kuomba, Yokebedi, na inaonekana kana kwamba Mungu hata hanisikii. Ninaomba na kuomba, na inaonekana kana kwamba Yeye anaziba sikio, hanisikii hata kidogo. Anaonekana kama hajali tena.”

⁸² “Sasa,” akasema, “tazama, Amramu, hilo halisikiki kama ni wewe. Wewe ni baba halisi, nawe. . . Hilo halisikiki kama ni wewe, kwa sababu sikuzote unatutia moyo, ukituambia kwamba tumwamini Mungu.”

⁸³ “Loo, lakini, mpendwa, ninapoomba sana, na bado Mungu hanisikii, na inaonekana kama kwamba inazidi kuwa mbaya wakati wote. Kadiri ninavyoomba, ndivyo inavyozidi kuwa mbaya.”

⁸⁴ Lakini, enyi wavulana na wasichana wadogo, je, Mungu husikia maombi? [Wavulana na wasichana wanasema, “Naam.”—Mh.] Yeye husikia maombi. Je, Mungu hujibu maombi? [“Naam.”] Naam. Je, anajibu haraka sana? Sio wakati wote. Sivyo? Hapana. Wakati mwingine anatufanya tungojee. Hiyo ni kweli? [“Naam.”] Lakini, Mungu hujibu maombi, sivyo? Na kwa sababu kila kitu kinakwenda kombo, hiyo siyo ishara kwamba tunapaswa kuacha kuomba. Tunaendelea tu kuomba, kwa vyovyote vile, sivyo? Hiyo ni kweli. Sasa, mumejibu vizuri. Mungu hujibu maombi. Hebu tuseme sote pamoja. “Mungu hujibu maombi.” Naam. Haidhuru hali ya mambo ikoje, Yeye hujibu, kwa vyovyote vile. Vema.

“Vema, unapanda kwenda kuomba tena?”

⁸⁵ “Naam.” Naye baba alikuwa na chumba cha siri huko juu kabisa darini ambapo alienda kuomba. Kwa hiyo anaingia pale usiku huo, anapiga magoti kando, akasema. . . Sasa akasema, “Yokebedi, sasa wewe nenda ukalale, wewe na hao watoto. Kwa sababu, msinisumbue, nitaomba labda usiku kucha usiku wa leo.”

⁸⁶ Kwa hiyo anapiga magoti, na anasali na kusali. Ninamwona akiinua mikono yake juu, na kusema, “Ee Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, kumbuka ahadi Yako kwa watu Wako! Sisi huku chini sana Misri, nasi tuko utumwani. Na, loo, wanyapara wetu katili wa—wanatusukuma kufanya mambo, na kutupiga kote, na watu wetu masikini wa—wanavuliwa nguo, na wanatuchapa kwa mijeledi. Na sisi ni watu Wako. Ee Mungu, hakika Wewe utasikia maombi! Hakika utajibu maombi! Nami ninaomba na ninaomba na ninaomba, na Wewe unaonekana kana kwamba hata hunijibu. Lakini, Mungu, ninaamini ya

kwamba Wewe ni Mungu, na hatimaye utajibua maombi.” Naye akaendelea kuomba namna hiyo, karibu usiku kucha.

⁸⁷ Basi kesho yake asubuhi, yapata saa tisa ama kumi, anashuka kwenye hivyo vipandio vidogo. Naye anaangalia kule, na huyo hapo maskini mke wake mpendwa, maskini Yokebedi. Alikuwa pale kitandani amelala. Nao maskini Haruni na maskini Miriamu walikuwa tayari wamelala kitandani, kwa hiyo walikuwa na usingizi tu jinsi walivyoweza kuwa, nao wamelala. Vema. Anamwambia... Akasema, “Kunachelewa, nawe unaninii tu...”

⁸⁸ “Naam, nimeomba usiku kucha.” Macho yake yalikuwa yametapakaa machozi, kwa sababu aliwalilia watu.

⁸⁹ Naye akasema, “Tazama, Amramu, hupaswi kuliendea kwa nguvu sana.”

⁹⁰ “Sasa,” akasema, “sikiliza, mpenzi. Hilo ni sawa. Lakini sasa angalia, una watoto wawili wa kulea hapa. Na mzigo ni wangu. Ikiwa mtu hatawaomba watu wetu maskini, itakuwaje kwao? Itakuwaje ikiwa mtu hawajali hawa watu? Mtu fulani hana budi kuomba.”

“Vema” anasema, “Amramu, huo mzigo sio wako wote.”

⁹¹ “Naam, inaonekana hivyo. Na kwa vyovyote vile, nitaomba, kwa vyovyote vile, wakati wote!”

⁹² Anaenda kazini siku hiyo. Na kila siku huja na kuondoka, na maskini taabu ile ile ya kale. Naye alikuwa na kazi ngumu. Ilimbidi... Walimwaga mota kwenye kalibu kubwa mno, naye ilimlazimu kusimama pale karibu na tanuru hiyo kubwa. Wakati wangeifungua, loo, jamani, karibu ingeipasua ngozi yake, joto hilo la kutisha! Angeyasukuma hayo matofali mle ndani na kuyaoka, kuyatoa; kujenga barabara kubwa mno, na minara mikubwa mirefu mno, kwa miungu ya sanamu na kadhalika. Naye huyu Mkristo halisi kule chini akifanya kazi namna hiyo, kwa adui. Lakini alikuwa mtumwa, alikuwa utumwani. Ilimbidi kufanya hivyo.

⁹³ Kila usiku akirudi nyumbani, angeomba. Na kupanda vipandio tena, na kuomba na kuomba na kuomba, na kurudi chini. Hakupata nafuu; mambo yaliendelea kuzorota.

⁹⁴ Basi siku moja kazini alisikia uvumi. Kasema, “Hiyo ni nini? Hiyo ni nini? Niambieni!” Mtu fulani alimnong’onezea mwingine. Baada ya muda kidogo, kabla siku haijapita, ilikuwa kote nchini, kitakachotukia.

⁹⁵ Ilikuwa ni nini? Baraza lilikuwa linaenda kukutana usiku huo. Maskini Mfalme Farao, yule mfalme katili wa kale atawaita watu wake wote pamoja, na kufanya baraza lingine kubwa. Kwa hiyo walikuwa na mkutano huu mkuu wa baraza kule chini.

⁹⁶ Kwa hiyo usiku ule akaingia, loo, alikuwa amekufa moyo kabisa. Anaingia, naye mkewe anasema, “Amramu, mpenzi,”

alikutana naye mlangoni na kumbusu, na kusema, “Nina chakula chako cha jioni kizuri na kina joto. Lakini,” akasema, “mpenzi, unaonekana umedhoofika sana. Kuna nini?”

⁹⁷ Kasema, “Loo, Yokebedi, laiti ungalijua kinachoendelea! Loo, ni kibaya kuliko hapo awali!”

“Ati nini?”

⁹⁸ “Sh-sh, siwezi kusema, watoto wako huku. Subiri hadi baada ya chakula cha jioni, nami nitakuambia juu yake.”

“Sawa.”

⁹⁹ Kwa hiyo, akaandaa chakula cha jioni. Basi akawapa chakula cha jioni, kisha kuwachukua watoto wote na kuwalaza kitandani.

¹⁰⁰ Basi, wakaingia ndani. Akasema, “Yokebedi, nataka kukwambia jambo fulani.” Kasema, “Moja ya mambo ya kutisha sana yanatokea.”

“Ati nini?”

¹⁰¹ Kasema, “Watafanya baraza lingine leo, usiku wa leo. Nao wakifanya hivyo, watatutwika mzigo mwingine sisi watu.”

¹⁰² Kwa hiyo, basi, hebu twendeni kwenye jumba la mfalme. Mfalme Farao anawatoa wote huko nje, na kusema, “Vema, ninyi majenerali wote! Mna shida gani hapa? Ninatoa maagizo yangu hapa! Watu hawa wanaongezeka kila wakati! Kuna nini? Je, hatuwezi kulikomesha hili?” Kasema, “Siku moja litakuja jeshi lingine humu ndani. Na hawa adui zetu wote, kutoka Gosheni kule, Waisraeli hawa, watajiunga na jeshi hili, nao watatushinda. Ndipo uchumi wetu mkuu utazorota, ufalme wetu mkuu utaangamizwa. Watatuchukua mateka. Mna shida gani? Zungumza, mtu fulani! Kwani hamjui la kusema?” Loo, alikuwa katili, na katili sana. Majemadari wote, wakitetemeka.

Mmoja wao akasimama, na kusema, “Nakutakia maisha marefu Mfalme Farao.”

“Vema, sema utakalo!”

¹⁰³ Kasema, “Mfalme na aishi maisha marefu. Mheshimiwa, bwana,” akasema, “Ningetamani kwamba ungewatwika hao watu mizigo zaidi.”

¹⁰⁴ “Baradhuli wee! Tayari mumewatwika mizigo mingi hao watu, na bado wanaongezeka. Mbona, wewe, ikiwa hayo ndiyo mawazo yote uliyo nayo, kaa tu nayo!” Loo, alikuwa mkali sana.

¹⁰⁵ Baada ya muda kidogo mmoja akainuka, tabasamu kubwa mno usoni mwake, kama ibilisi. Naye akasema, “Nakutakia maisha marefu Mfalme Farao.” Kasema, “Nina wazo.”

Akasema, “Vema, sema! Usisimame hapo namna hiyo!”

¹⁰⁶ Akasema, “Nitakuambia yale tunayoweza kufanya.” Kasema, “Unajua, watu hawa wanaongezeka haraka sana.”

¹⁰⁷ “Ndiyo, hiyo ni kweli!” Kasema, “Baadhi yao, baadhi ya watu wao hata wana kadiri ya watoto kumi na wanne, wakati mwingine wana watoto ishirini. Nao watu wetu hawana labda mmoja.” Kasema, “Wanaongezeka upesi sana, wanaifunika nchi nzima.”

¹⁰⁸ Unaona, Mungu alikuwa akifanya jambo fulani. Mnaona, Mungu daima humpumbaza ibilisi, mnaona. Mnaona? Anajua anachofanya. Mnaona? Na wanawake hawa wote wana watoto wengi tu.

¹⁰⁹ “Mbona,” akasema, “uishi maisha marefu ewe mfalme. Vema, hebu nikwambie. Kila mara mwanamke anapojifungua mtoto wa kiume... Tembea humu nchini ukawachukue wanawake ambao si... ambao si mama. Unaona, wanawake ambao kamwe hawakupata watoto, wanawake ambao hawataki watoto wala hawawapendi watoto, maskini wachawi wenye pua ndefu. Tazama, kadiri pua ilivyo ndefu, ndivyo alivyo bora zaidi! Maskini vidole vyao virefu, nyuso zilizopakwa rangi, ukawalete. Hawajui upendo wa mama ni nini. Kwa hiyo basi wakati mtoto mdogo wa kiume anapozaliwa, mbona, acha waende wakamchukue mvulana huyo mdogo, wamtoe nje na kukipasulia kichwa chake ukutani, na kumrushia mama nyumbani namna hiyo. Amtumbukize ndani ya kisima kirefu. Loo, bora zaidi, amtoe nje na kuifunga mikono na miguu yake, na kumtupa nje, na kuwanenepesha mamba. Hiyo ndiyo njia ya kumwondosha. Ndipo hawataongezeka sana, maana hakutakuwako na wanaume watakaosalia; watoto wote wa kiume wameuawa.”

¹¹⁰ “Loo,” Farao anasema, “hilo ni zuri! Hilo ni wazo zuri!” Mnaona ibilisi alivyo? Yeye ni mwovu, sivyo? Kasema, “Kwa hiyo hilo ndilo jambo la kufanya! Nenda kachukue... Unao... Sasa, kwa kuwa wewe ndiwe uliyekuwa na hilo wazo, nitakufanya tu kuwa mwangalizi wa hilo. Toka uende ukawachukue wanawake wazee wote unaowajua, ambao—ambao kamwe hawajawahi kuwa mama, wala hawapendi watoto. Nao ni...” Wao...

¹¹¹ Unaona, inahitaji mama kumpenda mtoto. Unakumbuka jinsi mama alivyokupenda? Vema, sasa unaona, mama anawapenda watoto wachanga.

¹¹² Lakini ilibidi wamtafute mtu ambaye—ambao hawakuwa... ambao hawakuwa na watoto, hawakutaka watoto, wa—wa—wanawake wakongwe katili kabisa. Kisha akasema, “Wafanye polisi. Basi unapowafanya polisi, na kuwapa amri kwamba wanaweza kuingia katika nyumba yoyote watakayo, na kumtoa kila mtoto mchanga na kupasulia kichwa chake ukutani, na kuwapa mamba wawale. Kila mtoto mchanga!” Loo, ukatili ulioje! Basi mnajua walichofanya?

“Sawa, hilo ni zuri!”

¹¹³ Ndipo kesho yake wakati Amramu alipokuwa kule chini akifanya kazi, alisikia kwamba mswada huo ulikuwa umetolewa.

¹¹⁴ Loo, anaenda nyumbani. Akasema, “Loo, Yokebedi! Loo, mpenzi, hebu nikwambie jambo fulani. Je, unajua ni agizo gani, lililotolewa? Kuwaua watoto wote wa kiume.” Ndipo akamwelezea. Kasema, “Jamani, siwezi kulivumilia.” Huyu akapanda ghorofani tena, kuomba. Usiku huo akaomba jinsi hajawahi kuomba hapo kabla.

¹¹⁵ Je, tunapaswa kuendelea kuomba? Loo, endelea kuomba! Hiyo ni kweli? Endelea tu kuomba, haijalishi ni nini kinachoendelea. Endelea kuomba!

¹¹⁶ Sasa, basi muda si muda mwajua, aliomba usiku kucha, “Ee Mungu, uturehemu! Tusaidie, Mungu! Tunaomba kwamba utatusaidia kwa namna fulani.” Huyu anashuka chini tena, kwenye mapambazuko.

¹¹⁷ Siku baada ya siku, na, loo, ni maombolezo ya jinsi gani kote nchini! Kila siku wangepasikia akina mama wakipiga mayowe, huku na huku mitaani. Wangewanyakua watoto wao wachanga kutoka mikononi mwao, watoto wao wachanga werevu wa kiume. Maskini hao wachawi wangeingia mle na, kuikamata miguu yao midogo, na kuwagongesha ukutani na kuwaua, na kuwatupia mamba. Maskini huyo mama angepiga magoti, naye angelia, “Loo, usimchukue mtoto wangu! Usimchukue mtoto wangu!” Na, loo, ni wakati wa jinsi gani waliokuwa nao!

¹¹⁸ Mnajua jinsi mama anavyompenda mtoto mchanga, na jinsi anavyowasukuma kidevuni. Kumbuka jinsi mama angekuchukua na—na kukuosha, na kukubusu, na—na—na angesema jinsi ulivyokuwa mzuri. Na jinsi alivyokulaza kitandani usiku. Na, loo, kama—kama ungeninii...mlango mdogo ungefunguliwa, upepo mdogo uingie, kitu kama hicho, loo, jamani, angekimbia upesi sana na kufunga mlango, amfunike mtoto mchanga, na, unajua, amchukue. Alikupenda. Unaona? Alikupenda. Loo, alipenda maskini kitu hicho kidogo ambacho Mungu alikuwa amempa, ambacho kilikuwa kinyonge wala kisingeweza kujisaidia, kwa hiyo alimpenda mtoto huyo mchanga. Naye aliwabusu tu watoto wake wachanga na kucheza nao, kwa sababu yeye alikuwa mama halisi. Mnaona?

¹¹⁹ Lakini wanawake hawa wazee wanaowaua watoto, hawakujua upendo wa mama ulikuwa ni nini. Hawakuwa mama. Yote waliyowazia, walikuwa tu na wakati mzuri akilini mwao, mambo ya ulimwengu, kwa hiyo wangeingia na kuwaua watoto hao wachanga. Wewe ni mdogo sana kujua, lakini yangali yanaendelea. Hiyo ni kweli. Sasa ninyi watu wazima mnajua ninachozungumzia. Hiyo ni kweli, mengi kupita kiasi! “Loo,” unasema, “nisingechukua...” Lakini kisa cha utoaji mimba ni kitu kile kile. Vema, lakini unaona hawajui upendo wa mama ni

nini. Sasa mnajua ninayomaanisha ninaposema “akina mama halisi!” Hiyo ni kweli. Hakuna tofauti; ibilisi yule yule! Kwa hivyo huko, basi, wao... Hebu wazia tu maelfu mara maelfu mara maelfu, kila mwaka, mbaya kama ilivyokuwa Misri, au mbaya zaidi.

¹²⁰ Na hapo, basi, waliingia, hawakuwa na upendo wa mama, kwa hiyo wangewachukua hao watoto wachanga na kuwaua. Lo, iliendelea kuwa mbaya zaidi na zaidi. Ndipo siku moja ukatokea uvumi mwingine, watafanya mkutano mwingine.

¹²¹ Farao akawaita pamoja washauri wake wote, wao, wote pamoja, wakaingia mle: kasema, “Vema, bado wanaongezeka! Tutafanya nini kuhusu hilo sasa?”

¹²² Maskini jamaa yuyu huyu mjanja, mwenye uso wa ibilisi, aliinuka. Akasema, “Mfalme Farao na aishi maisha marefu. Nina wazo. Angalia, unawafanyiza kazi wanaume. Unawafanya wawe na lundo la matofali, kiasi fulani kila siku, wafanye wayatengenezee kwa makapi. Umewaua wa—watoto wadogo na kadhalika, lakini bado wanaongezeka. Jambo unalopaswa kufanya, ni kuwaweka wanawake kazini, pia. Ikiwa utawaweka wanawake kazini, basi hawataninii...” Sasa, hapo si mahali pa mwanamke. Hapana. Basi wakasema, “Bali waweke wanawake kazini, na kuwaweka huko nje, na kuwaacha watengeneze matofali, pia. Ndipo watakuwa wamechoka sana watakapoingia, wao—hawawezi kuwapikia waume zao chakula cha jioni, hawawezi kuwa mama mzuri, mnaona. Na kwa hivyo ikiwa watafanya kazi na kuendelea hivyo, basi ha—hawataweza kufanya hivyo. Kwa hiyo, waweke kazini, pia.”

¹²³ “Hilo ni jema! Jamani, wewe ni mtu mwenye busara.” Kwa hiyo anawaweka wanawake wote kufanya kazi.

¹²⁴ Na huyu hapa maskini Amramu anakuja, akaingia usiku huo, kasema, “Loo, Yokebedi, sijui tutafanya nini. Sasa wanawaweka wanawake wote kufanya kazi. Na—nakwambia, jamani, sijui la kufanya! Sisi ni—sisi ni—sisi ni ninii tu... Sisi ni watumwa, na hali yetu inazidi kuwa mbaya zaidi na zaidi. Ni—ninabashiri hili: kama Mungu akipata kutufanyia lolote, itakuwa ni baada ya sisi sote kufa.”

¹²⁵ Sasa, Mungu hangojei hivyo, sivyo? Hapana. Mungu hututazama tu wakati mwingine, sivyo? Vema.

¹²⁶ Hivyo basi usiku huo, yeye alisema, “Ninapanda juu nikaombe jinsi ambavyo sikuwahi kuomba hapo kabla!”

¹²⁷ Sasa, hiyo ndiyo njia ya kuomba, sivyo? Omba kama vile hujawahi kuomba hapo kabla, maanisha kabisa! Unaona, ukipanda tu juu na kusema, “Bwana, mbariki *Fulani-na-fulani-na fulani*,” Mungu ha—havutiwi sana na hilo. Lakini ni wakati unapomaanisha kwelikweli! Ninyi wavulana na wasichana wadogo mnapoomba, mtilie maanani kabisa! Je, mnafanya hivyo shuleni? Je nyinyi hu—humwomba Mungu awasaidie shuleni?

Wakati—wakati unapoenda shuleni, na hupati gredi nzuri sana, wewe ingia na kusema, “Mungu, na—naomba unisaidie.”

¹²⁸ Huwa mnaomba? Ni wavulana na wasichana wangapi ambao huomba? Hebu tuone mikono yenu. Loo, hilo ni jema. Sasa, hilo ni jema. Je, una mahali pa siri unapoenda kuombea, ambapo mama na baba hata hawakuoni? Je, huwa mnomba hivyo? Ha—hamuombi hivyo? Uwe na mahali padogo, toka kisiri na uombe, nawe uombe maombi yako mafupi. Unaomba kila usiku kabla ya kwenda kulala? Unapoamka asubuhi, na kadhalika? Loo, hilo ni jema. Ni wavulana na wasichana wangapi wengine (inua mkono wako) ambao huomba? Huko juu kabisa jengoni. Loo, hilo si ni sawa? Vema, sasa, sasa, hilo ni jema. Hiyo inaonyesha kuwa una mama na baba halisi wanaokufundisha kufanya mambo haya. Sasa, sasa unapokuwa na haja kweli, afadhali uombe kwa uaminifu. Sivyo?

¹²⁹ Kwa hiyo, maskini Amramu, huyo anapanda ghorofani. Loo, jamani! Hakutaka chakula cha jioni. Alisema, “Ni vibaya sana. Jamani!”

“Loo,” alisema, “lazima ule chakula cha jioni, baba.”

“Kamwe siwezi kufanya hivyo, Yokebedi. Kamwe siwezi kula. Mimi—mimi. . .”

¹³⁰ “Loo,” kasema, “lakini unapunguza uzito, na una wasiwasi, na uso wako umedhoofika. Unatapika chakula chako, na kadhalika.”

¹³¹ “Loo, sijui la kufanya! Lakini,” akasema, “mpendwa, ikiwa mtu hatawahurumia watu moyoni, mtu asipowaombea watu, tutafanya nini? Tunazidi kunyanyaswa. Hakika, siku moja, Mungu atasikia!”

¹³² Naam, hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Mungu atasikia. Wewe maanisha na ukae hapo tu!

¹³³ Loo, wakati huu anapanda ghorofani tofauti. Wakati anapanda ghorofani wakati huu, anapiga magoti, anainua mikono yake hewani, anapiga makelele, “Mungu, ninazungumza Nawe sasa!” Amina. Kutilia maanani! “Mungu, Wewe unayo masikio, Nawe unaweza kusikia. Una macho, na unaweza kuona. Una kumbukumbu; unajua Neno Lako. Unajua ahadi Yako. Ninakusihi, Mungu, utazame hapa chini, Wewe ndiwe Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, ambapo watu Wako wako katika dhiki, nao wanakufa. Tutendee jambo fulani, Mungu! Inatubidi kuwa na Wewe mara moja! Inatubidi tu kuwa na Wewe, la sivyo tutaangamia. Lazima tuwe Nawe. Inatubidi kukupata, endapo tutaishi.” Hapo ndipo unapoomba kweli. Loo, aliomba!

¹³⁴ Unajua, wakati mwingine watu wanapoomba, wanachoka. Sivyo, mama na baba? Loo, unakuwa mchovu sana! Ndugu Branham wakati mwingine huchoka sana karibu nizi mie ninapoenda kuomba kwa muda mrefu; ninadhoofika tu, naenda

bila kula, na kadhalika, kwa siku kadhaa; na kuomba na kuomba na kuomba, na kuhubiri. Ndipo ninafikia tu mahali, nusura nizimie. Na wakati mwingine watu huwa hivyo. Huo sio wakati wa kukata tamaa. Endelea! Mungu atajibu! [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani mara tatu—Mh.] Naam, bwana. Endelea kushikilia! Naam, bwana.

135 Kwa hivyo anapanda vipandio vidogo vikuukuu vinavyokereza. Nami ninaweza kumwona Yokebedi akipita, na kusema, “Loo, Amramu, usifanye hivyo. Mpenzi, ni—ninaamini...”

136 “Sasa, Yokebedi, angalia, wewe ni mzuri, wa kupendeza...” Alikuwa mrembo, maskini mama mwenye sura nzuri. Naye akambusu shavuni, mwajua, na kumpapasa *hivyo*. Kasema, “Sasa, mama, wewe rudi ukawapeleke Haruni na—na mtoto Miriamu walale. Nami ninapanda kwenda kuomba. Na sasa, ukinisikia nikilia, usije huku juu tafadhali.”

137 “Vema, lakini, Amramu, utafanya nini, mpenzi? Karibu umekufa.”

138 “Ndiyo, lakini ni—nina mzigo wa watu moyoni mwangu. Inabidi nifanye jambo kuuhusu. Sina budi kukaa magotini mwangu. Na kwa hiyo watu wote...” Akasema, “Leo, leo hii tu, huko chini kwenye kilima cha matofali, nilikuwa huko chini, nikaendelea kusema, ‘Vema, hakika, Mungu atasikia!’ Ndipo mzee mmoja mkubwa akaja, akaweka mikono yake nyongani mwake, na kusema, ‘Kwani Yeye atasikia lini? Atasikia lini?’ Unaona jinsi watu hata wanaanza kuwa na uchungu? Wanampinga Mungu, kwa sababu wanaomba na kuomba na kuomba, wala hakuna kilichotokea. Na huyu anaomba na kuomba na kuomba, wala hakuna kilichotokea. Nao makuhani wote wanasema, ‘Siku za miujiza zimepita, na jambo pekee tunaloweza kufanya ni kuwaendea tu maskini hawa wanyapara wanaoabudu makafiri, au miungu ya makafiri, na kadhalika. Basi tufanye nini?’” Lakini akasema, “Lakini ninamwamini Yehova! Amina! Naamini angali anajibu maombi!”

139 Je, mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina!”—Mh.] Mnaamini hilo? Amina! Ninyi nyote mnaoamini hilo, semeni, “Amina.” [“Amina.”] Angali anajibu maombi! Vema.

140 Maskini mwili mnyonge, uliopoteza uzito mwingi sana. Huyu anapanda hivyo vipandio vinavyokereza, anaenda pale na kupiga magoti. Akasema, “Ee Yehova!” Loo, aliomba jinsi hajawahi kuomba hapo kabla! Akasema, “Yehova, tazama hapa! Wewe ni Mungu halisi. Tunaamini ya kwamba una masikio. Tunaamini una macho. Nawe unajua mambo yote. Nasi tunaamini Wewe ni Mungu wa Waebrania, nasi ni watu wa ahadi. Tunaamini Wewe hulitimiza Neno Lako.” Kasema, “Angalia hawa wapagani hapa, jinsi wanavyochukua kazi yetu ya bei rahisi, na kujenga barabara kuu na sanamu, na kila kitu.

Wewe, Yehova, je, ungeketi Mbinguni na kuwaruhusu wapagani wakutawale? Siamini utafanya hivyo.” Amina!

¹⁴¹ Bado siamini atafanya hivyo! Amina! Ibilisi anapoingia, Mungu angali ni Mungu! Kweli! Hatawaruhusu mashetani hawa kufanya hivyo. Ninaamini kwamba, siku hizi, ya kwamba wakati mitindo na ujinga, na upuuzi huu wote unapoendelea; bado, Mungu angali anatawala na Yeye angali ni Mungu! Kweli! Tunachohitaji ni mtu kama Amramu, aliye na mzungu moyoni mwao, ambaye atakaa hapo na kuliombea kabisa, mpaka Mbingu zitakapopasuliwa kule, Mungu akashuka na kujibu maombi. Amina.

¹⁴² “Sasa angalia hapa,” alisema, “Mungu, je, unawaacha makafiri wawadhihaki watu wako hivi? Majuma na miezi na miaka imepita. Tunaomba daima, kwa machozi, lakini... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Ee Mungu, utaruhusu jambo kama hilo?”

¹⁴³ Ninashangaa leo, kwamba wakati mamia ya watoto wachanga wanatupwa kwenye mito na mabwawa, pasipo kuruhusiwa kuishi, na visa vya utoaji mimba na kadhalika kufanywa; Ee Yehova, je, utaruhusu mambo kama hayo yaendele? [Ndugu Branham aligongagonga mimbarani mara sita—Mh.] Leo hii, wakati wiski na bia, na maisha ya usiku, na kila kitu, yanapopiga kelele. Na hata mimbara imedhoofika sana hata wanaogopa kusema lolote kuhusu jambo hilo. Yehova, je, utaruhusu upumbavu kama huo uendele? Atajibu siku moja. Loo, ghadhabu Yake inatisha inapokuja. Naam, bwana. Wanawake wakitoka nje na kufanya jicho la mtoto wao trei ya sigara, kudondoshea majivu, na kila kitu. Na watu wanawapeleka watoto wao wachanga kwenye vyumba vya bia, wasichana wadogo na wavulana wameketi, wenye umri wa miaka sita ama minane, wakinywa, na mambo kama hayo. Na taifa likiihalalisha, na “Ni sawa.” Loo, jamani! Je, mnafikiri kwamba Yehova haoni hilo? Wakati, hata wanawadhihaki watu ambao kwa kweli wako sahihi kwa Mungu. Mambo haya yote yakiendelea, kufanya dhihaka. Shikilia, endelea tu kushikilia! Yehova atajibu. Usijali. Vema.

¹⁴⁴ Twendelee mbele kidogo. Tunamkuta pale juu akiomba. Naye anachoka tu sana, anajilaza chini. Anaomba tu mpaka anaanguka sakafuni. Hawezi kwenda mbali zaidi, naye akalala kidogo. Akaamka. “Kuna nini? Angalieni hapa! Hiyo Nuru inatoka wapi? Loo, tazama, amesimama pale pembeni.” Hapo alisimama Malaika, upanga Wake ukining’inia ubavuni Mwake. Loo, akatazama tena, na akasugua macho yake. Akapiga magoti yake, akasema, “Bwana, loo, loo, u—ungetaka nini kwangu?”

¹⁴⁵ Akasema, “Amramu, Mimi ni Malaika wa Mungu. Nimetumwa kutoka Mbinguni, kukwambia Mungu alisikia maombi yako. Nami nimekuja kukwambia ya kwamba Yeye

atatuma mkombozi. Yeye huzikumbuka ahadi Zake zote.” Ninamwona Malaika sasa; mtazame, Anachomoa upanga huu. Anauelekeza kaskazini. Amramu akatazama. Akasema, “Kwenye ncha tu ya upanga huu mna ile nchi ya ahadi. Nami niliwaahidi Ibrahimu, Isaka na Yakobo, baba zenu, kwamba ninyi watu mtairithi nchi hiyo. Nami nimesikia kuugua kwa hao watu, nimesikia kilio cha watoto, nami nimeshuka. Nami nataka ujue ya kwamba utachukua sehemu kubwa katika hili, Amramu, kwa sababu ulikuwa mwaminifu katika maombi. Ulikuwa mwaminifu katika nyumba yako. Na yapata wakati kama huu mwaka ujao, Yokebedi, maskini mke wako mpendwa, atamkumbatia mtoto mchanga wa kiume. Basi huyo mtoto mchanga wa kiume atakuwa mkombozi.” Utukufu!

¹⁴⁶ Akasema, “Loo, naam. Naam. Loo, naam. Naam. Loo, Yeye ni mrembo sana.” Akatazama, ndipo Malaika akaanza kunyanyuka. Alionekana tu kama mbingu zote zilifunguka, Naye akatoka humo chumbani. Akasubiri kidogo. Akasema, “Loo, sijarukwa na akili.”

¹⁴⁷ Huyu akashuka kwenye vipandio, upesi sana, na kusema, “Yokebedi! Yokebedi, hima!”

Kasema, “Abe, kuna nini, mpenzi?”

¹⁴⁸ Kasema, “Keti!” Huku mwanga wa mwezi ukiangaza dirishani, ulikuwa... Alionekana mrembo. Naye akasema, “Nimemwona Malaika wa Mungu hivi punde, naye akaniambia mambo haya yote.”

“Loo, alionekana je?” akasema mama. “Alionekana je?”

¹⁴⁹ Kasema, “Loo, alikuwa wa kupendeza. Alikuwa amevaa vazi linalong’aa. Macho Yake yaling’aa. Naye alikuwa na upanga mkononi Mwake, ndipo akauelekeza kaskazini.” Hivyo ndivyo, mnajua, nchi ya ahadi ilivyo kutoka Misri; huko juu, Palestina. Akasema, “Aliuelekeza upande wa kaskazini. Naye alisema kwamba tutamzaa mtoto yapata wakati huu mwaka ujao, naye mtoto huyu mchanga atatokea kuwa mshindi, naye atawakomboha watu wake. Loo, halelu ya, Yokebedi!”

¹⁵⁰ Naye akaona kuwa alikuwa mweupe. Uso wake, alikuwa amekaza macho yake, macho yake makubwa yalikuwa yakitazama. “Yokebedi, kuna nini?”

“Loo, Amramu! Hapana, hapana, hapana! Tuna mtoto wa kiume?”

“Naam.”

¹⁵¹ “Loo, wewe... Haiwezekani. Unajua nini? Loo, laiti usingalipata ono hili. Unajua nini, Farao, anaua watoto wote wachanga.”

¹⁵² “Naam. Lakini, unajua, Mungu akitupa mtoto huyu, Mungu atamlinda huyo mtoto. Amina! Mungu aliahidi. Mungu atamshughulikia.”

153 Naam, kesho yake anatoka kwenda kazini. Na jamaa wote kule juu, wanamwona Amramu. Badala ya kuja, unajua, wote wakiwa wameinama chini na kuchoka, alikuwa ameinua mabega yake juu, akasema, “Pitisha matofali zaidi. Hima, twendeni!”

“Kuna nini?”

“Utukufu kwa Mungu! Mungu atajibu maombi.” Loo, hakuna...

154 Unajua, inakufanya ujisikie vizuri unapopata jibu. Hivi hatujui hilo, enyi baba na mama, Mungu anapotoa jibu? Si lazima uone ono. Ujue tu jibu lipo, hamna lingine. Hamna lingine, kujua tu jibu lipo.

155 Sasa, sikilizeni kwa makini sasa, ninawatakeni msikilize, kilichotokea. Sasa mwajua, baada ya kitambo kidogo, alisema, “Vema, Amramu, una shida gani?”

156 “Mungu atajibu maombi! Mungu atajibu maombi!”

“Vema, atajibuje maombi?”

“Hilo halileti tofauti yoyote.”

157 Mzee mmoja akajongea, na kusema, “Sasa unafikiri atawahi kujibu lini?”

158 “Vema, sitakwambia, kwa sababu wewe ni asiyeamini, hata hivyo. Nipitishie matofali mengine.” Akayatupa mle ndani namna *hiyo*...?...Usijali; si lazima uwaambie wasioamini mambo yote, sivyo? Hailleti tofauti yoyote. La, bwana. Bila shaka sivyo. “Nipitishie matofali mengine. Haleluya! Atajibu maombi!” Hivyo ndivyo unavyojisikia unapojua itatokea. Sivyo? Naam, bwana.

“Vema, atafanyaje jambo hilo?”

159 “Hujui, kwa vyovyote vile, kwa hivyo endelea tu kupitisha matofali.” Wakayaweka yote mle ndani, wakayaweka hayo matofali yote ya kale mle ndani.

160 Usiku huo akaenda nyumbani, akasema, “Loo, Yokebedi, wazia hilo, tutapata mtoto! Loo, atakuwa ndiye mkombozi! Mungu atamtuma. Loo, litakuwa jambo la ajabu.”

“Lo, lakini mimi ni ninii sana...”

161 “Loo, acha kuhangaika! Acha kuhangaika! Jamani! Mungu ame—Mungu ametega masikio sasa. Mungu yuna masikio; Mungu anaweza kusikia. Mungu ana mikono; anaweza kukomboa.” Kwa hiyo, loo, alikuwa na imani nyingi sana.

162 Unajua, unapoomba kabisa, unapata jibu, hakika unapata imani nyingi sana basi. Loo! Umewahi kuombea chochote, nawe unajua Mungu atakutimizia? Je, ninyi wasichana wadogo mnafanya hivyo, nanyi wavulana wadogo? Naam. Hakika. Hapo ndipo Yeye... Hapo ni wakati unapojua itatokea. Vema.

¹⁶³ Mwaka mzima unapita. Na muda si muda mwajua, huyu hapa Amramu anakuja kutoka kazini siku moja. Basi ilikuwaje? Mtoto mchanga mwenye sura nzuri kuliko wote, loo, alikuwa ni kipenzi mdogo, mrefu *hivi*. Na hivyo akamchukua, akamkabidhi Amramu. Naye akambusu, mnajua. Anampenda, unaona. Naye mama alikuwa amemshika. Loo, ni hazina iliyoje! Akasema, “Loo, ninaogopa sana, hata hivyo, unajua. Maskini mtoto huyu mchanga, yeye ni kipenzi mdogo wa kuvutia.”

¹⁶⁴ Na unajua nini? Biblia ilisema huyo alikuwa mtoto mchanga mwenye sura nzuri sana aliyepata kuzaliwa. Sasa najua akina mama watatofautiana nami katika hilo. Uh-huh. Walidhanja. . . Mama yako alidhanja wewe ndiye mtoto mchanga aliye mwenye sura nzuri kuliko wote. Sivyo? Naam. Anayo haki ya kuwazia hilo. Lakini Biblia ilisema huyu alikuwa mtoto mchanga mwenye sura nzuri. Loo, alikuwa kito. Mungu alikuwa ameweka mikono Yake juu yake, mwajua. Kwa hiyo, loo, alikuwa kitu kidogo kirembo sana! Angelala pale, naye—naye angetabasamu tu kidogo, bila meno.

¹⁶⁵ Hukuwa na ndugu mdogo na wengineo, wangelifanya hivyo, wakati ha—hakuwa na meno, anatabasamu tu *hivyo*?

Na muda si muda mwajua, “Ng’ee!”

“Loo, jamani, masalaale! Whiu! Najua, hebu tumfiche tu.”

“Kuna nini? Unafanya nini?”

¹⁶⁶ “Mpeleke chumba cha chini. Unajua agizo ni nini. Unaona, kama hao wachawi wenye pua ndefu wakija hapa, watamchukua mtoto wetu mchanga na kumwua. Hiyo ni kweli. Hatuwezi kumwacha alie.” Kwa hiyo, loo, alihitaji—alihitaji kiamshakinywa kidogo ama chakula cha jioni. Kwa hiyo mama anampeleka pale pembeni, anamnyonyesha, mwajua. Na kwa hivyo alikuwa sawa wakati huo.

¹⁶⁷ Kwa hivyo siku kadhaa usiku baada ya hapo, walikuwa wakicheza naye, na, “Ng’ee!” Huyo akalia tena, mwajua, akaanza kulia. Huyo akaondoka upesi sana, na kumficha—kumficha upesi namna hiyo. Na chumba cha chini, kule chini nyuma kabisa, ukutani, Amramu alikuwa ameandaa mahali padogo ambapo angeweza kumficha huyo mtoto mchanga.

¹⁶⁸ Ndipo basi muda si muda mwajua, walisikia kitu ghorofani kikifanya. . . [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] *Whiu!* Wakatoroka! Kila mtu alitawanyika mahali pamoja, kasema, “Ndio hao. Hao ni wale wachawi wazee, wenye maskini vidole virefu, makucha yaliyopakwa rangi!” Nao wale wachawi wa kale. . . Akatazama chini pale, na kuchungulia dirishani, akasema, “Naam, hao ndio. Wamesimama pale.”

[Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.]
“Jiwekeni wazi!”

169 Mzee Amramu akatoka nje, akafungua mlango, akasema, “Mnataka nini?”

170 Wakasema, “Mna mtoto mchanga humu ndani, nasi tunajua hilo. Nasi tutamchukua.”

“Hatuna mtoto wa kuwapa.” Hawakuwa naye.

171 “Tutaingia na kuangalia, kwa vyovyote vile. Sisi ni polisi wanawake. Unaona beji zetu?” Na hiyo ni...Je, hicho si ni kitu cha mwanamke kuwa? Lakini, “Sisi ni polisi wanawake. Tumepata haki zetu kutoka kwa utawala!” Unajua, tunao hapa sasa. Na hivyo—hivyo basi wanashuka, wanaingia. Wanaingia ndani na kupindua sofa, na kufungua droo zote, na kutupa kila kitu sakafuni, na kuchukua nguo zote za kitanda na kuzikung’uta. Kisha wanapanda ghorofani na kuona ambapo baba alikuwa na mahali padogo pa siri. Wakaangalia kila mahali, lakini wasingeweza kumpata huyo mtoto mchanga.

172 Wasingeweza kumpata huyo mtoto mchanga, hivyo wakamwendea huyo mwanamke pale, maskini—maskini Yokebedi amesimama pale, uso wake ulikuwa mweupe. Wakamwendea, wakasema, “Tazama hapa! Tunajua kuwa wewe u—umejifungua. Tunaweza kujua kutokana na vile unavyoonekana. Tunajua wewe ni mwanamke anayenyonyesha, nasi tunajua mtoto huyo yuko hapa. Tutarudi. Tutampata!” Hao wakatoka nje ya mlango. Wakaufunga mlango kwa kishindo, nao hao wakatoka nje.

Akasema, “Loo, loo, tufanye nini? Tufanye nini?”

173 Basi Amramu akasema, “Omba.” Je, hilo ndilo jambo la kufanya? [Wavulana na wasichana wanasema, “Naam.”—Mh.] Je, hilo ndilo jambo? “Omba! Na tuombe.”

“Loo, loo, loo! Sijui la—la kufanya. Loo!”

174 Kwa hiyo akasema, “Sasa, angalia, wewe tulia, kisha uende ukamnyonyeshe mtoto tena. Ninapanda ghorofani nikaombe.”

175 Kwa hiyo anapanda ghorofani na kuomba. Akasema, “Yehova, Wewe una masikio. Yehova, una macho. Yehova, unaweza kusikia. Unaweza kujibu maombi. Ulitupa mtoto huyu. Ulitupa ahadi Yako. Nawe utatimiza ahadi Yako, Nawe utamtunza mtoto huyo mchanga. Nami nina imani!”

176 Baada ya kuomba, kuchoka sana, a—alianguka tu *hivi* akalala. [Ndugu Branham anaigiza kukoroma—Mh.] Alikuwa amechoka sana! Alifanya kazi mchana kutwa, na kuomba usiku kucha. Alikuwa amechoka. Basi mnajua kilichotokea? Alilala, akaota ndoto.

177 Mnajua, Mungu hunena katika ndoto, pia, sivyo? Hakika, Yeye hufanya hivyo. Ndiyo, Yeye hufanya hivyo. Anaweza. Mnaona? Naye hunena katika ndoto.

¹⁷⁸ Loo, alipoamka, alisema, [Ndugu Branham anadata kidole chake mara moja—Mh.] “Jambo ndilo hilo! Nilipaswa kufikiria hilo. Hilo ndilo ninalopaswa kufanya.” [Ndugu Branham aligongagonga mimbarani mara tano.] “Kamwe sitasema chochote juu yake.”

Huyo anashuka kwenye vipandio. Akasema, “Yokebedi!”

“Abe, mpenzi? Loo, nimechoka sana. Siwezi kulala.”

“Loo, nenda ukalale. Nenda ukalale. Yote yamekwisha.”

“Unajua?”

“Loo, najua tu. Nina imani!”

¹⁷⁹ Badala ya baba, usiku huo, kupanda ghorofani kuomba, alishuka kwenye chumba cha chini. Alikuwa na shughuli nyingi kule chini. Nashangaa alikuwa akifanya nini. Hebu twende chini kisiri tumwone. Ninamwona kule chini, akifanya... [Ndugu Branham anaanza kuvumisha, na kugongagonga huku akiigiza ujenzi wa kitu fulani—Mh.] “Pum, pum, pum.” [Ndugu Branham anavumisha.] Chukua unyasi huu, na uchunguze tena, usokote uone kama ni mzuri. [Ndugu Branham anavumisha.] Maskini Haruni alitoka nje siku hiyo, na kukusanya kifurushi kizima mikononi, akakiweka kwenye chumba cha chini, mwajua. [Ndugu Branham anavumisha wimbo.] “Mungu anakutunza.” [Ndugu Branham anavumisha wimbo.] “Dini ya mtindo wa kale, yote haina budi kuwa ni kweli!” [Ndugu Branham anatwaga kitu fulani.] Ifungeni kote.

Alisema, “Amramu, una shida gani?”

“Haleluya! Hakuna, mpenzi. Endelea.”

¹⁸⁰ [Ndugu Branham anavumisha—Mh.] “Ni dini ya mtindo wa kale.” [Ndugu Branham anatwaga tena.] “Ni dini ya zamani.” Lete hii *hapa*, mwajua. “Ni dini ya mtindo wa kale.” “Shhhhhhh,” ziba yote. “Na ni nzuri vya kutosha kwangu! Nipe hii ya kale...” Alikuwa akifanya kitu fulani.

¹⁸¹ Mnajua, baada ya juma moja au mawili kupita, muda si muda mwajua, walishangaa alichokuwa akifanya.

¹⁸² Kwa hiyo usiku mmoja wakati wote walipokuwa wamelala, yeye alipanda kisiri ghorofani na kukileta kitu hiki kidogo, mwajua. Anakiinua *hivi*. Naye anakileta. Anainua kifuniko ambapo Yokebedi mkewe amelala, halafu anakiingiza chini ya hicho kifuniko. Nao mtoto Haruni na—na mtoto Miriamu walikuwa wamelala, mwajua; loo, alikuwa mtoto mdogo mzuri sana, huyo msichana mdogo alikuwa, na vivyo hivyo mtoto Haruni. Kwa hiyo, akakiweka chini pale. Akasema, “Yokebedi, mpenzi.”

¹⁸³ Akasema, “Je, umekuwa katika chumba cha chini ukiomba wakati huu wa usiku, Amramu?”

Kasema, “La. Nimekuwa katika chumba cha chini, nikimsifu Mungu.”

Kasema, “Umekuwa ukifanya nini?”

184 Kasema, “Nataka kukwambia. Sasa, unajua maskini hao wachawi wanarudi.”

“Naam.”

185 “Nami ninataka kukwambia tutakachofanya. Tume kuwa na huyu mtoto mchanga sasa kwa miezi mitatu, na hatuna budi kumwondosha.”

“Loo, Amramu! Ati huna budi kufanya nini?”

“Hatuna budi kumwondosha huyu mtoto mchanga.”

“Ati kumwondosha huyu mtoto mchanga?”

“Naam.”

“Loo, katili wee!”

“Hapana, mimi si katili. La, la, la. Najua ninachofanya.”

186 “Una maana gani? Mbona, utakuwa katili kama Farao. Ati unataka kumwondosha mtoto wetu?”

“Naam, nitamwondosha huyu mtoto mchanga.”

“Loo, hatuwezi!”

187 “Sasa sikiliza. Tukibaki naye, tutampoteza. Na tukimpa Yule aliyetupa, Yeye atampata.” Hiyo ni kweli? “Sasa, ukimzuilia, tutampoteza.”

“Je, utampotezaje?”

“Mbona, maskini hao wachawi watapitia hapa na kumchukua.”

188 Pia angalia, ukiizuilia nafsi hiyo na kuendelea na kuishi kama walimwengu, utaipoteza. Wachawi wa kuzimu wanakufuata wewe. Na hiyo ni kweli. Upumbavu huu wote wa kale wa ulimwengu na kadhalika huko nje, unakuandama moja kwa moja. Ukiizuilia, utaipoteza; lakini ukimrudishia Yule aliyekupa, utaipata na kuihifadhi. Ni kitu gani sasa? Tukiizuilia, tunafanya nini? [Watoto wanasema, “Tunaiipoteza.”—Mh.] Tunaiipoteza. Tukimpa Kristo, tunafanya nini? Tunaihifadhi. [“Tunaihifadhi.”] Amina! Hilo ni jema. Sasa mumejibu vizuri.

189 Sasa yeye akasema, “Yokebedi, tutampoteza kama tukibaki naye. Kwa hivyo kama tuki—tukimrudisha kwa Yule aliyetupa, basi tutamhifadhi.”

190 Sasa unayo nafsi. Na, baba na mama, ninyi vivyo hivyo. Lakini ukiizuilia, utaipoteza. Hiyo ni kweli. Wachawi wa kuzimu wataichukua. Wote wanaiwinda! Lakini ukimrudishia Yule aliyekupa, utaihifadhi hata Uzima wa milele. Haleluya! Amina! Samahani, enyi watoto, mimi—mimi ni wa mtindo wa kale tu vya kutosha kupaza sauti. Ukiizuilia . . . Hebu tuseme hivyo, sote

pamoja: [Kusanyiko linakariri pamoja na Ndugu Branham—Mh.] “Ukiizuilia, utaipoteza; ukimrudishia Yule aliyekupa, utaihifadhi.” Amina. Kumbuka sasa, mpe Yeye.

¹⁹¹ Sasa hebu tuangalie. Loo, akaanza kulia. Akasema, “Loo, utafanya nini naye?” akasema.

“Angalia hapa, nataka kukuonyesha kitu fulani.”

“Una nini chini ya kitanda changu pale?”

Kasema, “Hebu nikuonyeshe.” Naye akakichomoa.

“Lo, ni kikapu kidogo cha manyasi!”

¹⁹² Ni meli ndogo, ndivyo ilivyo. Haina usukani, haina tanga, haina mizinga juu yake, na ingali itapakia shehena ya thamani sana ambayo imewahi kupakiwa na meli, kufikia wakati huo. Sikia! Haina nahodha wala wafanyakazi. Ndugu, najua Meli ya mtu mzima, kama hiyo, pia!

¹⁹³ “Loo,” akasema, “Am- . . . ngoja niitazame, Amramu, hebu nione.” Anaenda hapa.

¹⁹⁴ Kasema, “Angalia hapa, ina kifuniko kidogo juu yake. Unaona?” Anakiinua hicho kifuniko kidogo.

Alisema, “Whiu! Inanuka vibaya! Ah! Whiu! Salale!”

Kasema, “Naam, inanuka.”

“Kwa nini?”

¹⁹⁵ “Niliimiminia lami kwelikweli. Yote imepakwa bereu, kote.” Bereu ni lami, mwajua, kwa hivyo waliipaka bereu kila mahali. Hiyo ndiyo aliyokuwa akichemsha hapa chini, na kuimwaga juu ya manyasi haya. Alikuwa ameipaka bereu. Kasema, “Unaona, maji hayawezi kuingia kuvuja ndani yake. Unaona, imezibwa kote.” Kisha kasema, “Wala hayawezi kupenya ndani yake, maji hayawezi. Niliipaka bereu.”

Kasema, “Whiu! Inanuka vibaya!”

¹⁹⁶ Ninyi watoto mnajua lami ni nini, wakati wanapotengeneza barabara, “Loo, harufu mbaya hiyo!” Lakini i—i—i—inazuia . . . I—inaziba nyufa zote barabarani. Na hivyo ndivyo hii inavyofanya, inayazuia maji yote.

¹⁹⁷ Na hivyo ndivyo maombi humfanyia mwaminio. Hayo ndiyo kila siku hukuinga na ulimwengu, ni wakati unapojipaka bereu kwa magoti yako, na kusema, “Bwana Yesu!” Nayo hiyo Damu inateremka, nayo inakuziba kabisa kusudi ibilisi asiweze kukupata. Unaona? Hiyo ni kweli. Unaona? Kwa hiyo basi, loo, mara nyingi watu huzunguka na kusema ni baya sana, lakini, hilo halileti tofauti yoyote, linakuweka salama. Hilo ndilo jambo muhimu, kuwa salama. Kasema, “Wewe ni wa mtindo wa kale,” lakini, hilo halijalishi, linakuweka salama.

“Vema,” kasema, “tutafanya nini?”

198 “Sawa,” kasema, “Nitakwambia tutakalofanya. Tutamchukua huyu mtoto mchanga, na tutakuwa na kuachana kidogo. Nasi tutamchukua huyu mtoto mchanga na kumweka humu ndani, na kumweka huko nje katika Mto Nile.”

199 “Loo! Hapana! Hapana! Hapana! Amramu, huwezi kumweka mtoto wetu huko mtoni.”

200 “Ndiyo! Ndiyo! Ninajua ninachofanya.” Unaona, alikuwa ameota ndoto, alijua la kufanya. Unaona, Mungu alikuwa amemwagiza. Alijua la kufanya. Alijenga hii, naye akaona ilikuwa ni mfano ule ule wa ile safina iliyomwoko Nuhu huko nyuma katika wakati wake.

201 Kwa hiyo akasema, “Tazama hapa, nimetoboa tundu dogo juu yake, apate kupumua. Unaona, kusudi aweze kupata mwanga wa jua kupitia humo.”

202 Nanyi mnajua, safina katika Biblia ya Kale, zamani za kale, ilitengenezwa vivyo hivyo. Nayo ilikuwa na shimo mumo humo juu yake, kusudi upate kuona ndani, unaona, na mahali ambapo ingembidi kuangalilia juu.

203 Kwa hiyo basi maskini mtoto huyu mchanga, asiyepelewa jina, hata hakuwa na jina lolote; maskini mtoto mchanga asiye na jina, na hata hivyo ni mtoto mchanga mwenye sura nzuri kuliko wote ulimwenguni.

204 Kesho yake usiku, walipoingia, nao wakangoja hadi yapata saa tisa alfajiri, ndipo wao... Anaenda kule. Naye amemaliza kuomba. Akaenda kule, naye akasema, “Sasa njoo, Yokebedi, amka!”

205 Na kwa hiyo wakawaamsha watoto Haruni na Miriamu. Loo, akaja huko na kuweka mikono yake, akasema, “Baba!” Mtoto Miriamu, akasema, “Hutamchukua ndugu yetu mdogo, mtoto mchanga, sivyo, na kumweka kwenye Nile walimo maskini hao mamba wote?”

206 Naye akazirudisha nyuma maskini nywele zake namna *hiyo*. Na ninii yake... Alikuwa na macho mazuri, na maskini nywele za kupendeza. Na hivyo akambusu shavuni. Akasema, “Mpenzi, inaniumiza, pia. Inaniumiza, pia, lakini lazima tufanye hivi.”

207 Mnaona, enyi wasichana wadogo na wavulana, wakati mwingine inatubidi kufanya mambo ambayo kwa namna fulani yanatumiza, lakini lazima tuyafanye, kwa vyovyote vile. Wakati wasichana wanaposema, “Hei, umewahi kuvuta sigara?”

Utasema, “Hapana.”

208 “Vema, jaribu moja! Loo, mimi ni rafiki msiri wako, unajua. Naam, hebu ijaribu.”

209 Lakini wewe, inaweza ikakuumiza kidogo, lakini sema, “Huh-uh. Siitaki.” Unaona? Unaona? “Sitaki.”

Kasema, “Je, utakuja, twende tukaone sinema leo jioni?”

210 “Hapana, hapana. Huh-uh. Siendi kwenye sinema.” Unaona? Huenda ikaumiza kidogo tu. Unaona?

211 “Loo, wewe hujachanuka bado.” Usiamini hilo. Huenda likaumiza kidogo tu. Achana nalo; ndilo jambo lifaalo kufanya, unaona. Daima fanya hivyo, fanya jambo lifaalo. Vema.

212 Na sasa wakati hao wasichana wanapojifunza maskini upuuzi huu wa kucheza dansi kwa vidole vya miguu namna hiyo, nao wanakutaka ufanye hivyo; wewe waambie, “La, la.” Usifanye hivyo, unaona.

213 “Loo, vema, ni furaha nyingi.” Hujali ni burudani kiasi gani. Unataka kufanya yaliyo mema, kwa hiyo sikuzote unafanya yaliyo mema. Sasa, kumbukeni hilo tu sasa. Hamtalisahau, sivyo?

214 Sasa, sasa walifanya nini? Walimchukua mtoto huyo mchanga basi, na wakapanda kule. Ndipo mtoto Haruni akajongea, akasema, “Baba, kwani utafanya nini na mtoto wetu mchanga?”

215 Akasema, “Haruni, keti hapa pajani mwangu, kipenzi.” Kasema, “Angalia, Haruni. Kama tukimshikilia huyu mtoto mchanga, tutafanya nini?” [Kusanyiko linasema, “Tutampoteza.”—Mh.] “Tutampoteza. Lakini tukimrudisha huyu mtoto mchanga mikononi mwake Yeye aliyetupatia sisi, tutafanya nini?” [“Tutamhifadhi.”] “Tutamhifadhi.” Hiyo ni kweli.

“Lakini utafanyaje, baba?”

216 “Sijui. Sijui jinsi litakavyofanywa, lakini Mungu atalifanya.” Unaona?

217 Na kwa hiyo basi wakamwingiza huyo mtoto mchanga mle ndani, naye huyo akaenda. Na hapa wanaenda sasa, wanaelekea mlangoni. Wanashuka kwenda mlangoni, anatazama *huku* chini mtaani, *kule* chini mtaani. Hakuna mahali, hakuna mtu anayekuja. Kasema, “Njoo, Yokebedi. Njoo, Haruni. Njoo, njoo, Miriamu. Hima twendeni.”

218 Wanakichukua hicho kisafina kidogo na kushuka mtoni kwenye majani marefu. Loo, ni muda mrefu sana kabla ya mapambazuko. Naye huyu hapa mtoto Haruni anakuja, kule nyuma amemshika mtoto Miriamu, ndugu na dada wadogo, walikuwa wakilia. Na maskini Yokebedi, anatembea pale, akasema, “wooi, woori, woori, woori.”

“Sh-sh-sh-sh-sh! Wanachungulia mtaani. Jihadhari. Sh! Jihadhari.” Wanashuka mtaani. “Sh-sh-sh! Jihadhari.” Wamembeba mtoto mchanga. Naye mama alikuwa amembeba huyo mtoto mchanga, na—na baba amekibeba kile kisafina.

219 Wanafika mtoni. Loo, ni mto mkubwa sana, karibu wa pili kwa ukubwa ulimwenguni. Na kwa hiyo, basi, mto mkubwa sana, na mwepesi, na uliojaa tu mamba wakubwa mno na

ngwena. Loo, walikuwa wanono. Whiu! Walikuwa wamewala hao watoto wadogo wote. Walikuwa wanono tu. Na—naye anasema, Yokebedi anamwambia Amramu, mumewe, akasema, “Loo, vipi kama mamba watamkamata? Vipi kama mamba humu ndani watamgusa?”

²²⁰ Kasema, “Usijali. Wakithubutu kuweka pua zao kwenye lami hiyo, watatimua mbio, unaona. Hiyo ndiyo sababu inanuka, unaona. Atainua pua yake juu,” kasema, “asingeweza kusikia harufu ya mwili wa binadamu, kwa hiyo ataondoka. Lami hiyo itanuka vibaya sana hata watakimbia. Itakuwa sawa. Usijali.” Hivyo wao... Na hapo wakakiweka chini, kile kisafina. Naye akasema... “Sasa mnyonyeshe mtoto.”

²²¹ Kwa hiyo mama anamchukua mtoto na kumnyonyesha, naye anamnyonyesha mtoto mpaka anapopata kiamshakinywa chake, asubuhi na mapema. Ndipo basi [Ndugu Branham anatoa sauti ya busu—Mh.] anambusu. Na kusema, “Sasa, Haruni, unaweza kumbusu.” Naye Haruni anambusu. Kisha anampelekea Miriamu, naye anambusu. Naye mama anambusu, na, “Loo,” akasema, “Nilininii tu...”

²²² “Sasa, sh-sh-sh! Sasa sikilizeni, hatuna budi kuwa askari. Mnaona? Hatuna budi kuwa askari. Sasa nyote mnataka kumbusu tena?” Wote wanambusu, wote, tena. Kisha wanamlaza humo ndani.

²²³ Naye mama alishona blanketi ndogo, akamfunika, na kijimto. Akakiweka mle. Akasema, “Kitoto changu kipendwa, Mungu akubariki.”

“Sh-sh-sh! Sasa, Mungu atalishughulikia hilo. Usijali.”

²²⁴ Akafunga hicho kijifuniko. Na muda si muda mwajua, baba anaanza kuvua koti lake, na kuvua shati lake. Huyu hapa anakwenda, akienda kwa shida majini.

²²⁵ Mnafikiri ni nini kinachoendelea Mbinguni, kuhusu wakati huu? Haleluya! Mnajua, mambo yanapoendelea huku chini, kuna jambo fulani linaloendelea Kule juu, pia. Amina! Ninaweza kumwona Mungu akiinuka kutoka kwenye Kiti Chake cha Enzi, anajongea, anasema, “Gabrieli! Gabrieli! Uko wapi?”

Gabrieli anasema, “Mimi hapa, Bwana.”

²²⁶ “Njoo hapa! Nitakuonyesha jambo fulani!” Kasema, “Enyi Malaika wote njoni hapa, kwa dakika moja, ninataka kuwaonyesha jambo fulani. Ninao watu wanaoniamini Mimi. Ndiyo, ninao watu wanaonitumainia. Njoni hapa, dakika moja! Ni vyema kwenu Malaika wote, liangalieni hili. Tazameni!”

“Liko wapi?”

“Kule chini kabisa. Tazameni.”

“Naam, naam. Naam, naliona.”

227 “Tazameni kule chini. Mnaona nchani mwa yale—yale—yale manyasi kule, hayo majani marefu na kadhalika?”

“Naam.”

“Mnaona kule!”

“Ni kitu gani?”

228 “Kuna mtu aliyeinua mikono yake hewani, amepiga magoti, akiniita. Kuna mama anayelia, na watoto wawili wadogo wanaolia. Wananitumainia Mimi hadi mwisho kabisa. Gabrieli, unakumbuka ulipoingia? Unamkumbuka mtu yule?”

229 “Ndiyo, nilikutana naye chumbani usiku huo na kuzungumza naye. Uh-huh.”

230 “Bado ananiamini Mimi. Ninao watu wanaoniamini Mimi! Ninao watu ambao wataniumini Mimi hata mwisho!” [Ndugu Branham anagonga-gonga mimbarani mara sita—Mh.] “Unamwona? Mwangalie.”

“Ndiyo, loo, si ni ushujaa huo!”

231 Baba anatembea majini, anaanza kukisukuma maskini kijimashua hicho nje.

Ninaweza kumsikia akisema, “Gabrieli!”

“Ndiyo, Bwana?”

232 “Waite Malaika elfu kumi jukwaani. Wape amri ya kwenda vitani mara moja. Yaite majeshi ya Mbinguni. Wapeleke wote juu-chini, kwenye ngazi za Mbinguni, na uwapange wote kando-kando ya Mto Nile. Ninaamuru kwamba hakuna mamba atakayeigusa shehena hiyo! Hakuna kitakachoigusa! Usiruhusu hata kipande kinene cha kuni kukikaribia.” Haleluya!

233 Gabrieli akasema, “Itatekelezwa.” Jamani! Akapiga parapanda! Malaika elfu kumi wakaja na silaha!

“Rubani. Utakuwa wapi, Bwana?”

234 “Nitakuwa upande wa pili.” Yeye daima huwa kwenye maeneo ya mashambulizi makali. “Nitasubiri upande ule mwingine. Nina kusudi. Watu wanaponiamini Mimi, nina kitu fulani, kusudi fulani; itakuwa sawa nao.” Vema, Yeye anaenda upande huo mwingine.

235 Namwona Musa...ama mtoto Haruni na hao wengine, wakirudi mtaani, wakilia. “Sh-sh-sh-sh-sh! Kitazame.”

236 Na mtoto Miriamu, angali amesimama, akitazama. Akasema, “Loo! Loo!”

237 Kasema, “Njoo huku, Miriamu, kunapambazuka. Hima, jogoo wanawika kumekucha. Hima, kunapambazuka. Hima, kipenzi, haya twendeni!”

238 Kasema, “Loo, baba, baba! Tafadhali, mara moja zaidi. Acha nisimame tu, acha tu niweke doria nione kitakachotokea. Nitarudi nyumbani baada ya kitambo kidogo.”

239 “Loo,” [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] “hilo ni wazo zuri, Miriamu. Huenda ikawa ni sawa. Wewe simama tu uone kitakachotukia.”

“Sawa, nita—nitakiangalia.”

240 “Sasa, harakisha uje nyumbani baada ya kitambo kidogo. Angalia tu kitakachotukia. Ndipo uje, utupashe habari, yale yanayoendelea.”

“Sawa, baba.” Nao hao wakaenda zao, ilibidi waharakishe.

241 Mtoto Miriamu, anasimama na anatazama. Muda si muda mwajua, kunapambazuka. “Loo, loo, loo, ni nini hicho kinachokuja huko? Ni—ni kipande kinene. Hapana. Yule ni mamba? Loo, aligeuka.”

242 Ha-ha! Aliona nini? Aliona kile ambacho watu wengi hawaoni. Mnaona? Shehena ile ndogo ilikuwa ikienda, ikielea pale. Walidhani haikuwa na rubani yeyote; walidhani haikuwa na nahodha yeyote. Ilikuwa naye. Wote walikuwa wamekusanyika pande zote.

243 Huyu hapa maskini mamba anakuja, anasema, “Loo, angalia pale!” Huyu hapa anakuja, akielea namna *hiyo*. Anaenda... Loo, hapana. La, la. Hawezi kuikaribia shehena ile.

Mle ndani alisimama mwenye kukomboa, mkombozi, Wayahudi milioni tatu waliohitaji kukombolewa. [Ndugu Branham anagonga-gonga mimbarani mara tano—Mh.] Ibilisi wote kuzimuni wasingeweza kumgusa. Kikielea chini, maskini kisafina hiki kidogo cha kale kilichotengenezwa kwa lami, kikishuka mtoni.

244 Muda si muda mwajua, kinaingia kwenye mzunguko wa maji. “Loo!” Miriamu akasema, “Loo! Loo! Angalia ule! Ule mzunguko wa maji, uangalie! Ungalie hivyo!” Muda si muda mwajua, mara moja ukaondoka tu.

245 Hivyo ndivyo unavyokwenda. Tunaingia kwenye mzunguko wa maji, wakati mwingine, maskini jahazi hili dogo. Usijali. Kuna Mtu anayeangalia. “Malaika wa Mungu hufanya kituo wakiwazunguka wamchao.” Ana elfu kumi ya hao kwenye mwendo wa kijeshi sasa.

246 Mtoto Miriamu, anashuka, anapanda juu ya mwamba huu mkubwa, na kukimbia juu yake namna *hii*. Naye anashuka mbio, anakiangalia kile kisafina. Na kushuka chini kupitia *hapa*, na kupitia kwenye lundo hili la majani marefu. Baada ya kitambo kidogo kinakwama huko nje. Kasema, “Loo! Loo, nashangaa!”

247 (Sasa, baba yake alimwambia, kasema, “Sasa usiache mtu yeyote akuone ukikiangalia hicho. Mtu akitokea, jifanye tu kana kwamba hata hukiangalii, pitia tu kwa njia nyingine. Usi—usijifanye kana kwamba unaangalia hata kidogo, endelea tu kwenda mbele.” “Vema,” alisema.)

248 Anashuka kwenda ufukoni. Kinakwama. Muda si muda mwajua, kuna kundi kubwa la wavuvi. Naye anajifanya tu kana kwamba yeye ni msichana mdogo tu anayetembea pale. Yapata, saa nne mchana sasa, mwajua, kwa hiyo aliteremka tu mtoni. Naye anaendelea kuangalia nyuma kwa jicho lake, kwa upande, aone kinakoenda.

249 Baada ya muda kidogo anapita kundi lingine. Anaendelea tu kuangalia; anasonga mbele kidogo. Anasonga mbele, akienda mbele kidogo.

250 Baada ya kitambo kidogo anafika kwenye ukuta mkubwa sana. “Loo, jamani, inaingia nyuma ya ukuta huu!” Afanye nini? Hajui la kufanya. Kwa hiyo hawezi kuruka huo ukuta, hivyo basi anaingia tu majini na kukanyaga juu yake namna *hii*, na kutambaa juu. Anafika pale, kisha anaendelea kutembea.

251 Muda si muda mwajua, yuko kwenye bustani ya kupendeza. Maua yanachanua kila mahali, na ni nzuri sana. Sasa sikilizeni kwa muda kidogo tu. Sasa angalieni, enyi wasichana wadogo. Maua mazuri, na, loo, miti yote imekatwa ikasawazishwa. Ilionekana nzuri sana! Ni bustani. “Loo,” akasema, “angalia kule, kile! Loo, jamani! Niko kwenye bustani ya ikulu, ikulu ya Farao, bustanini. Nitafanyaje hapa? Kama wakinipata hapa ndani, loo, jamani, watanifanyia nini?”

252 Naye akaangalia. Hicho hapo kisafina kinakwenda, na kwa namna fulani kinasimama mle majini, na kinaanza kuelea huku na huko, nje majini. Sijui kwa nini. Ndipo anamsikia mtu fulani akizungumza. Anarudi kujificha vichakani. Akaketi, na kuangalia nje namna *hiyo*, unajua, mtoto Miriamu akaanza kuchungulia, apate kuona.

253 Muda si muda mwajua, hawa hapa wanaume wakubwa weusi wenye nguvu wanakuja wamebeba kanopi juu namna *hii*. Na wajakazi wakifuatana nao, nao wanaimba. Na huyu hapa mwanamke mmoja anakuja, naye amefunga mkanda mkubwa wa dhahabu kichwani mwake, wenye nyoka mkubwa mdomo wazi (namna *hiyo*) mbele yake. Naye ni mwanamke mwenye sura nzuri, naye anashuka. Amevikwa majoho mazuri sana, na kadhalika. Ndipo ninasikia mmoja wa hao wajakazi akisema, “Mtukufu, unafikiri maji yatakuwa na joto asubuhi ya leo?”

254 Miriamu akasema, “Ati mtukufu? Loo, huyo hana budi kuwa ni wa jamaa ya kifalme, kwa hivyo lazima niko bustanini. Nao wakinikamata humu ndani, watanifanyaje?”

255 Vema, anashuka, nao watu hawa wakubwa weusi waliobeba nguzo namna *hii*, wanashuka ukingoni mwa mto namna *hiyo*, naye anavua viatu vyake. Basi mjakazi mmoja alikuwa na taulo, na wengine walikuwa na sabuni. Naye alikuwa akishuka apate kuoga asubuhi. Kwa hiyo anashuka kule chini na kuanza ku—kujiandaa apate kuoga. Anavua viatu vyake. Akasema,

“Nitachovya vidole vyangu majini nione kama yana joto bado. Loo, ni mazuri tu, ninii tu . . . Ni kitu gani hicho pale nje?”

256 “Loo!” Miriamu, maskini Miriamu akasema, “Loo! Loo, amekwisha kukipeleleza kisafina kile.”

“Loo,” akasema, “huyo ni mamba?”

257 Mmoja wa wale wanaume wakubwa wenye nguvu alisema, “Hebu kidogo, nitajua.” Pwa, pwa, pwa, anatembea humo majini. Anakichukua *hivi*, anaingia. Kasema, “Mtukufu!” Anampa mjakazi. Naye huyo mjakazi anakichukua na kumkabidhi yeye namna *hiyo*, naye anakiweka chini.

258 Akasema, “Ni kitu gani? Whiu, kinanuka! Kina lami kote. Angalia hapa, kina shimo juu yake.”

259 Naye Miriamu akasema, “Loo! Loo, huyo hapo maskini ndugu yangu anaenda! Huyo hapo maskini ndugu yangu anaenda!”

260 Na kwa hivyo wanakifungua *hivi*. “Loo, ilikuwa ni mtoto!” Naye akaanza. . . Mtoto mchanga mwenye sura nzuri kuliko wote ulimwenguni! Na, loo, Mungu Ambaye angeweza kusababisha chuki, angeweza kusababisha upendo; na upendo wote ambao angeweza kuuweka katika moyo wa mwanadamu, wa mama kwa mtoto, aliweka katika moyo wa msichana huyo. Basi yeye—yeye akasema, “Ni mmojawapo wa Waeb- . . . Najua ni nini. Ni yule babangu katili! Yeye ni katili sana! Aliagiza hao watoto wadogo wote wa Kiebrania wauawe. Na mmoja wa hao akina mama amemtupa mtoto wao mchanga, akitarajia atatua popote pale. Loo, yeye ni mwovu! Vema, hatamwua huyu, kwa sababu huyu ni wangu.” Uh-huh, mnaona jinsi Mungu anavyofanya?

261 Akamnyanyua, na [Ndugu Branham anatoa sauti ya busu—Mh.] anambusu. Ndipo mtoto akalia. Basi alipolia, aliuchangamsha tu moyo wake. Akasema, “Maskini mtoto mchanga.” Kasema, “Nitamchukua na nitamwita . . . Nitampa jina.” Na hapo ndipo alipopata jina lake.

262 Jina lake lilikuwa nani? [Kusanyiko linasema, “Musa.”—Mh.] Musa. Nalo *Musa* maana yake ni “aliyetolewa majini.” Mnaona?

263 Akasema, “Sasa nitamwita Musa, naye atakuwa mtoto wangu mwenyewe. Nitamtunza. Lakini sasa,” akasema, “lakini mimi ni mwanamwali, siwezi kumnyonyesha. Si—si—sina njia ya kumlisha.” Hawakuwa na chupa hizi na kadhalika. Wanawake hawakuvuta sigara kama wanavyofanya siku hizi, unaona, na kujitia sumu. Kwa hiyo akasema, “Vema, kama mnajua . . .” Kasema, “Ni—nitafanyaje?” Kwa hiyo akasema, “Mimi . . .”

264 Mmoja wao akasema, “Nitakwambia, mtukufu, nitakutafutia mama wa kumnyonyesha mtoto wako.”

“Loo,” akasema, “hilo ni sawa kabisa.” Maskini . . .

265 Kitu fulani kikazungumza, Malaika aliyesimama pale kichakani, kasema, “Miriamu, hiyo hapo nafasi yako! Hiyo hapo nafasi yako!” Mtoto Miriamu akatimua mbio. Kasema, “Kamwe usiseme kitu sasa, usijitambulishe. Nenda kule ukaseme ‘utamtafuta mlezi,’ ndipo uende ukamlete mama yako.”

Vema, kwa hiyo akasema hivyo. Akasema “Mtukufu!”

266 Sasa, kwa kawaida, angesema, “Kwani unafanya nini humu ndani?” Lakini, mnaona, Mungu alikuwa akiyafunika hayo yote. Kwa nini? Alikuwa na Malaika elfu kumi wakienda kijeshi. Mnaona? Mpango Wake utafanikiwa. Alikuwa na Malaika elfu kumi wamesimama pale.

267 Kwa hiyo muda si muda mwajua, kasema, “Mtuku- . . .”

Kasema, “Naam, kipenzi, unafanya nini hapa?”

268 Akasema, “Nimekuona tu hivi punde na mtoto mchanga.” Kasema, “Najua mahali aliko mama mzuri ambaye angekulelea mtoto wako mchanga.”

269 Akasema, “Hima, nenda ukamlete, na umwambie kwamba nitampa dola mia tatu kwa juma kwa kumlea mtoto huyu, kisha nitampa seti nzima ya vyumba huko kwenye ikulu. Na kama unajua palipo na mwanamke wa Kiebrania, ambaye ni mama wa kunyonyesha, anayeweza kumnyonyesha mtoto huyu, huyu ni mtoto wangu.”

Kasema, “Naam, mtukufu, nitakuletea mmoja.”

270 Kasema, “Sasa, ngoja kidogo! Kabla ya kuingia kwenye kasri, huna budi kujua nenosiri. Unaona, hujui nenosiri. Kila siku tunalo nenosiri. Sasa, nenosiri leo hii, unajua lilikuwa ni lipi? ‘Uma na mzigo wa nyasi kavu.’” Kasema, “Hivyo ndivyo unavyopaswa kusema upate kupitia langoni.”

271 Kwa hiyo maskini Miriamu anashuka mbio kwenda nyumbani, upesi alivyoweza kwenda, akiruka ukuta, chini mitaani, na kushuka *huku*, na kushuka *huku*, na upesi awezavyo kwenda. Akakimbia nyumbani.

272 Na—naye Amramu alikuwa amefika nyumbani hivi punde tu, na Yokebedi. Na, loo, walikuwa na huzuni, wakishangaa ni nini kinachoendelea. Akasema, “Maskini mtoto wangu! Maskini mtoto wangu!” Yeye. . .

273 Akasema, “Sasa sikiliza tu.” Kasema, “Nimepitia kule chini mtaani hivi punde tu, na maskini mama yule amemweka kila mtu macho siku nzima. Wamepitia ujirani huu asubuhi ya leo, nao wamekipasua kichwa cha kila mtoto aliyekuwako katika ujirani.” Kisha kasema, “Jinsi walivyokuwa wakipiga mayowe na kulia! Sasa, sijui, mtoto wako, popote alipo. Alipo mtoto wetu, Mungu atamlinda.”

274 Mara tu kitu kikafanya. . . [Ndugu Branham anagonga-gonga mimbarani mara nne—Mh.] “Loo! Loo! Hao hapo,

mlangoni sasa.” Kwa hiyo, wakaenda na kuangalia. Hapana, sio. Ilikuwa ni Miriamu.

275 Akasema, “Loo! Loo, Miriamu! Ingia, kipenzi! Imekuwaje kwa mtoto?”

Akasema, “Mama, nina njaa sana.”

Kasema, “Lakini mtoto amepatwa na nini?”

276 Akasema, “Nafa kwa njaa, mama.” Kasema, “Loo, Bwana asifiwe! Haleluya! Nusura nife kwa njaa, mama.”

Kasema, “Lakini imekuwaje kwa mtoto?”

277 Kasema, “Mama, ninaumwa na njaa sana ningeweza kula kila kitu nyumbani.”

278 Kasema, “Tutakuletea chakula, lakini imekuwaje na mtoto?” [Ndugu Branham anagonga-gonga mimbarani mara tatu—Mh.]

279 Kasema, “Loo, mtoto hajambo, mama. Nipe chakula. Loo, nina furaha sana!”

“Lakini imekuwaje kwake?”

280 “Vema, nipe chakula, nusura nife kwa njaa.” Ungeweza kuwazia hilo?

281 Akasema, “Miriamu! Huyu ni mama na baba yako. Yuko wapi mtoto?” [Ndugu Branham aligonga-gonga mimbarani mara tatu—Mh.]

282 Akasema, “Mama, nilikwambia. Mtoto, nilimwona, na yuko salama. Sasa, mama, nipe chakula; nafa kwa njaa. Unajua, nu—nusura nife kwa njaa.” Kama mlivyo mnaporudi nyumbani kutoka shuleni, mnajua; loo, inabidi tu upate kitu.

Kwa hiyo, akaenda akamletea sambusa. Kasema, “Sasa niambie.”

283 Naye anafanya, “Yum, yum, yum,” akila, mwajua, hivyo. Kasema, “Mama?”

Kasema, “Naam, lakini ilikuwaje kwa mtoto?”

284 “Mbona,” kasema, “mama. . .” Akamsimulia hadithi. Kisha kasema, “Mama, nenda kachukue nguo zako zilizo bora sana, na uchukue sanduku lako, maana unaenda kumlea mtoto.” Loo! Loo! Loo!

“Ati nini?”

285 Ukiipoteza, utaipata tena. Hiyo ni kweli? Ukiizuilia, utaipoteza. Ukiitoa, uipoteze, utaipata. Je, hiyo ni kweli?

286 Naye maskini Miriamu anaendelea tu kula. Kasema, “Naam.” Kasema, “Unaenda ikulu leo. Isitoshe, bali unaenda, utapewa, utapewa dola mia tatu kwa juma, na vyumba bora zaidi nchini, kumlea mtoto wako mwenyewe.”

287 Mara ya kwanza katika historia yote ya ulimwengu ambapo mama aliwahi kulipwa amlee mtoto wake mwenyewe. Mnaona

jinsi Mungu anavyolifanya? [Ndugu Branham anapiga makofi mara tatu—Mh.] Haleluya! Kumlea mtoto wake mwenyewe, na kupata dola mia tatu kwa juma kwa ajili yake, na vyumba bora zaidi nchini. Mungu hufanya mambo, sivyo? Je, kuomba kuna faida? [Kusanyiko linasema, “Ndiyo.”] Je, ni vizuri kuomba? [“Amina.”]

²⁸⁸ Kwa hiyo, aliandaa sanduku lake dogo. Tutaharakisha sasa, tutafunga katika dakika moja. Kwa hiyo sisi . . . Akaandaa sanduku lake, naye huyo akashuka barabarani, upesi tu alivyoweza kwenda. Na muda si muda mwajua, akaja; maskini mlinzi mkubwa amesimama pale na mkuki wake mkubwa, kasema, “Ni nani huyo?”

Akasema, “Uma na mzigo wa nyasi kavu.”

“Pita.” Unaona jinsi Mungu anavyofanya mambo?

²⁸⁹ Akamwendea mlinzi mwingine. Huko akauchomoa upanga wake, akasema, “U nani wewe? Ni nani huyo anayepita?”

Kasema, “Uma na mzigo wa nyasi kavu.”

Kasema, “Pita.” Jamani! Mnaona jinsi Mungu anavyofanya mambo?

²⁹⁰ Anapanda juu, anaenda kuiangalia ikulu; anaanza kupanda, ndipo walinzi wote wa kifalme wanatoka, wanachomoa panga zao. “Ni nani huyo anayepita?”

Kasema, “Uma na mzigo wa nyasi kavu.”

“Pita uingie ndani.”

²⁹¹ Muda si muda mwajua, mtu akatokea, akasema, “Je, wewe ndiwe maskini yule mwanamke ambaye mtukufu malkia anangojea?”

“Ndiyo.”

²⁹² “Na huyu ndiye mama wa kumnyonyesha mtoto mchanga aliyepatikana asubuhi ya leo?”

“Ndiyo.”

²⁹³ Kasema, “Naam, mwingize ndani.” Kwa hivyo anamleta mtoto mchanga ndani . . . au anamleta mama ndani.

²⁹⁴ Ndipo—ndipo ma—maskini binti mfalme akatoka nje, akasema, “Je, unajua chochote kuhusu watoto wachanga?”

Akasema, “Naam, mtukufu.”

Akasema, “Mwangalie mtoto huyu. Je, si anapendeza?”

“Naam, mtukufu. Naam.”

Kasema, “Je, unaweza kujua jinsi ya kumlea mtoto?”

“Naam, mtukufu. Hakika.”

²⁹⁵ “Vema,” wakasema, “Nitakupa, mshahara wako ni, dola mia tatu kwa juma.” Hum! Hivi Mungu hakuwa mwema? Kisha akasema, “Nawe umepata vyumba bora zaidi katika ikulu, na

chakula chako utaletewa. Hata haitakulazimu kutoka na kupika chakula chako mwenyewe.” Kasema, “Sasa, huyu hapa mtoto, kuwa mwangalifu. Usimwangushe.”

“Loo, usijali, sitamwangusha. Usijali, sitamwangusha.”

“Mpe malezi mazuri sana.”

²⁹⁶ “Usijali, nitampa. Atakuwa na malezi yaliyo bora zaidi.” Hakika, alikuwa ni wake mwenyewe, mnaona. “Nitampa malezi yaliyo bora kabisa.”

“Unaona ni mtoto wa kupendeza?”

“Mwenye sura nzuri sana,” akasema.

“Vema.”

²⁹⁷ Huo mlango ukafungwa, nyuma ya Miriamu, na mama yake, na mtoto Musa. Ndipo mlango ulipofungwa, alitazama pande zote. Akasema, “Tsk-tsk-tsk! Na alidhani wewe ni mtoto *wake* mchanga. Ha-ha-ha-ha-ha!” Loo, jamani! Akampapasapapasa.

²⁹⁸ Alikuwa amefanya nini? Yeye... Kama angemzuilia, angefanya nini? [Kusanyiko linasema, “Angempoteza.”—Mh.] Maana, alimrudishia Yule aliyempa, naye (nini?) akampata, naye anaweza kumhifadhi. Sasa itakuwaje tukiipoteza... Tukizuilia nafsi yetu, inakuwaje? [“Tutaiipoteza.”] Tutaiipoteza. Na tukimrudishia Yeye Yule aliyetupatia, itakuwaje? [“Tutaiihifadhi.”] Tutaiihifadhi. Je, hiyo ni kweli?

²⁹⁹ Ni wangapi wenu nyote mngetaka kuja kuyazunguka madhabahu na kuomba? Je, mngependa kufanya hivyo? Je, ungependa Yesu akutunze kama alivyowatunza wao, mtoto mchanga? Vipi... Hebu sote, watoto wadogo, tukusanyike kuyazunguka madhabahu hapa sasa. Je, mtafanya hivyo? Njoni moja kwa moja, pigeni magoti kuyazunguka madhabahu. Na tuombe, ninyi nyote. Watoto wote wadogo sasa njoni huku. Mliipenda hadithi yangu kuhusu hili? [Kusanyiko linasema, “Naam.”—Mh.] Je, mliipenda hiyo? Vema, sasa njoni moja kwa moja kuyazunguka madhabahu. Sasa njoni. Ninyi wote watoto wadogo njoni, pigeni magoti moja kwa moja kuzunguka madhabahu, piga magoti tu pale penye—pale pale madhabahuni. Jambo ndilo hilo. Ninyi watoto wote mlio huko nyuma, njoni hapa sasa, tutaomba. Sawa. Unataka kuja huku na kuomba. Njoo upige magoti madhabahuni. Hiyo ni sawa. Sasa, hilo ni jema. Hiyo ni sawa tu.

³⁰⁰ Sasa, akina mama, mnataka kuja, pia, na akina baba, nyote mnataka kupiga magoti kwenye marefu ya kanisa?

³⁰¹ Sasa nataka kuwauliza ninyi watoto wadogo jambo fulani hapa. Tazama. Je, unaamini kwamba Yesu anakupenda kama vile alivyompenda Musa? Je, unaamini kwamba Malaika wanakulinda hivi? Sasa, Mungu alikupa nafsi, sivyo? Sasa, ukiizuilia nafsi yako, itakuwaje kwake? [Watoto wanasema, “Utaipoteza.”—Mh.] Utaipoteza. Lakini kama utamrudishia

Yesu asubuhi ya leo, basi utafanya nini? [“Utaihifadhi.”] Uta—utaihifadhi. Unataka kuokoa. Sasa unataka kuiokoa nafsi yako, sivyo? Nanyi mnataka kukua kuwa mama halisi na wanawake halisi, sivyo; na mwanaume halisi, wahubiri, na kadhalika? Je, hutaki kufanya hivyo? Sasa, ukitaka kufanya hivyo, basi mpe Yesu nafsi yako. Hivi ndivyo unavyofanya. Unasema, “Yesu Mpendwa, hii ndiyo yote niliyo nayo kukupa, ni nafsi yangu, bali Wewe nilinde kama vile ulivyomlinda Musa.”

³⁰² Sasa, kama baadhi yenu watu wazima mnaotaka kuja kupiga magoti, pia, baadhi yenu akina mama, labda, kwamba huenda mkataka kupiga magoti hapa asubuhi ya leo. Vema, mmekaribishwa pia. Mkipenda, njoni, pigeni magoti papa hapa. Hilo ni sawa. Huyu hapa mama anakuja na mvulana wake mdogo. Je, mwingine atakuja?

³⁰³ Baba, dadi, yeyote kati yenu, kama unataka kuwa mtu wa maombi kama Amramu alivyokuwa, njoo, piga magoti, pia.

³⁰⁴ Mama, kama unataka kuwa kama Yokebedi, mbona, njoo moja kwa moja, piga magoti, pia.

³⁰⁵ Hakika, ni kwa kila mtu. Maana (Nini?) una nafsi, pia. Ukiizuilia, itakuwaje? [Kusanyiko linasema, “Utaipoteza.”—Mh.] Utaipoteza. Na ukimrudishia Yule aliyekupa, itakuwaje? [“Utaiokoa.”] Utaiokoa, kwa Uzima wa milele. Hiyo ni kweli. Sasa, je, hivi hamtakusanyika huku, ninyi nyote mpendao sasa, na tufanye maombi pamoja na watoto hawa wadogo, na pamoja nasi, pamoja na wote sasa.

³⁰⁶ Siku ya Mama, siku ya ajabu. Na labda usiku wa leo, huenda nikabadili somo langu na kuendelea usiku wa leo na kuelezea kile ambacho mama huyo alifanya, jinsi mama huyo alivyofanya. Yeye ndiye aliyemsomesha mvulana wake mdogo kuwaongoza Israeli wote hadi kwenye nchi ya ahadi. Loo, alikuwa mama halisi. Hivi hakuwa mama halisi? [Watoto wanasema, “Ndiyo.”—Mh.] Sasa, una mama halisi, pia, naye mama anakuombea. Alikuwa baba halisi. Na baba anakuombea. Na sasa sote tutaomba pamoja, na kumwomba Yesu atusaidie.

Ndugu Neville, waweza kuja, upige magoti pamoja nasi?

³⁰⁷ Na sote tuinamishe vichwa vyetu, kila mahali. Sasa Dada Gertie. . . [Mpiga piano anaanza kucheza *Waleteni Ndani*—Mh.]

³⁰⁸ Mpendwa Baba wa Mbinguni, hadithi hii ndogo, rahisi leo, kuhusu zamani za kale, ambapo baba na mama wa kweli, mwaminio wa kweli, alikuja Kwako na wakakuabudu. Walikuamini Wewe. Kulikuwako na dhiki nchini wakati huo. Na tunajuaje ya kwamba hakuna maskini Musa wa kisasa anayepiga magoti hapa asubuhi ya leo! Tunajuaje ya kwamba hakuna mtoto Miriamu mdogo wa kisasa aliyepiga magoti hapa asubuhi ya leo, pia, nabii mke!

309 Ee Baba Mpendwa, hawa watoto wadogo wanakupenda, nao wanakuja, wakipiga magoti msalabani, wakitambua ya kwamba wana nafsi ambayo haina budi kuokolewa, nao wanakupa hiyo Wewe sasa. Kwa maana tumesoma hivi punde katika Neno Lako, “Ukiipoteza, utaipata; na ukiizuilia, utaipoteza.” Na, Baba, hawataki kuzuilia nafsi zao. Hawataki kuishi kwa njia yao wenyewe. Wanataka kutoa nafsi zao Kwako, ili kwamba, kwa kuitoa, wapate Uzima wa Milele. Jalia, tujalie, Bwana.

310 Wabariki hawa wavulana na wasichana wadogo wote walio madhabahuni. Wabariki mama na baba walio hapa asubuhi ya leo. Ee, neema na rehema Zako ziwe juu yao wote. Utusamehe, Bwana, dhambi na kupungukiwa kwetu kwote. Ondoa magonjwa kati yetu.

311 Tuma Malaika! Haleluya! Mungu, Wewe uliyemwamuru Gabrieli, na Malaika elfu kumi wakaenda kijeshi, ni Malaika wangapi zaidi waliokuja walipowaona maskini watoto hawa wakipiga magoti kwenye madhabahu hii asubuhi ya leo! Pande zote, juu ya madhabahu hii na humu kanisani, wamesimama Malaika wa Mungu. Malaika anayerekodi yuko hapa, akiandika majina yao katika Kitabu. Wanapoteza nafsi zao, ili waweze kuipata katika Kristo! Tujalie, Bwana.

312 Jalia, tangu leo hii, na kuendelea, maisha yao madogo yawe matamu na manyenyekevu. Na wawe watoto watiifu kwa wazazi wao na kwa Baba yao wa Mbinguni, hata siku utakapowaita Nyumbani. Waongoze katika jahazi lao dogo, chini kupitia kila mzunguko wa maji. Kila wakati linapokwama vichakani, naomba Malaika wa Mungu walisukume kwenye mkondo wa upendo wa Mungu. Tujalie, Bwana. Na mwisho wa safari, jalia wapate Makao ya upendo, na mama yao na wapenzi wao huko Utukufuni, ambapo Mungu anasimama langoni kukaribisha, siku hiyo. Tujalie, Baba.

313 Utusamehe dhambi na makosa yetu yote. Na utusaidie tangu leo hii tuwe Wako kabisa. Tunawakabidhi watoto hawa wadogo mikononi Mwako sasa. Na akina mama hawa pamoja nao, Bwana, ya kwamba watakuwa akina mama wafaa katika Siku hii ya Akina Mama, wakati huu wa ukumbusho ambao hutolewa kwa akina mama. Na jalia, tangu leo, wawe mama bora. Jalia watoto wawe watoto bora. Jalia sisi sote tuwe bora zaidi, Bwana, na tukutumikie Wewe zaidi. Utujalie, Baba, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa hebu tuimbe pambio dogo.

314 Je, unaamini Yesu alikuoka? Je, unataka Yesu akulinde sasa unaposimama? Inua mkono wako Kwake, namna *hii* sasa. Ninataka uwageukie baba na mama, na hao wote. Geuka *hivi*. Sasa tazameni hapa, mama na baba. Nyinyi wasichana na wavulana wote simameni. Sasa, ni wangapi wanaomkubali Yesu kama Mwokozi wenu, na mtamwamini Yesu tangu sasa na

kuendelea, kukutunza kama alivyomtendea mtoto Musa, hebu tuone mikono yenu ikiinuliwa. Kila mmoja wenu. Hilo ni jema! Sasa ilikuwaje? Ukiizuilia nafsi yako, utafanya nini? [Kusanyiko linasema, “Utaipoteza.”—Mh.] Utaipoteza. Lakini ukimpa Yesu, itakuwaje? [“Utaihifadhi.”] Utaihifadhi. Sasa, vipi kama Yesu amekupata sasa asubuhi ya leo? Na wewe ni wa Yesu sasa, sivyo? Wewe ni mvulana na msichana mdogo wa Yesu.

³¹⁵ Waangalie jamaa hawa wadogo wamesimama hapa na machozi. Waniambia Mungu hajui hilo? Amina. Wanaume na wanawake wa kesho! Simameni.

Waleteni kutoka maeneo ya dhambi;

Waleteni, waleteni,

Waleteni watoto wadogo kwa Yesu.

Loo, Jinsi Ninavyompenda Yesu, sasa njoni!

Loo,

Nyote.

. . . jinsi ninavyompenda Yesu,

Tuinue mikono yetu juu sasa.

Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,

Loo, jinsi ninavyompenda Yesu,

Kwani alinipenda kwanza.

³¹⁶ Si ni mzuri huo? Sasa, *Yesu Anawapenda Watoto Wadogo Wa Ulimwengu*. Tupe sauti, dada. Sasa ninyi nyote geukeni moja kwa moja hivi, kwangu, ninyi wasichana wadogo. Nataka kuimba *Yesu Anawapenda Watoto Wadogo Wa Ulimwengu*. Ni wangapi wanaoujua? Vema, hebu tuimbe sasa.

Yesu anawapenda watoto wadogo,

Watoto wote wa ulimwengu;

Wekundu na wa manjano, weusi na weupe, ni
wa thamani machoni Pake,

Yesu anawapenda watoto wadogo wa
ulimwengu.

³¹⁷ Sasa, ninyi nyote mko kwenye jeshi sasa. Je, mlijua hilo? Mnajua mko katika jeshi la Mungu? Sasa, niangalieni moja kwa moja sasa. Na muuimbe huu pamoja nami sasa, maana ninyi ni askari sasa. Mnajua hilo? Askari wa msalaba! Sasa, *Huenda Nisitembee Kijeshi*. . . Mnajua huo? Vema. Vema, muda mrefu uliopita, wimbo wa kale wa shule ya Jumapili niliojifunza.

Huenda kamwe. . .

Sasa ninyi, pamoja nami sasa. [Ndugu Branham anaashiria huku akiimba *Niko Katika Jeshi La Bwana*—Mh.]

Huenda kamwe nisitembee na jeshi la miguu,

Nisipande farasi, nisirushe mizinga;

Huenda kamwe nisiruke juu ya adui,

Lakini niko katika jeshi la Bwana.

Niko katika jeshi la Bwana,
Loo, niko katika jeshi la Bwana!

Njoni pamoja nami sasa. Sote pamoja sasa. Sasa!

Huenda kamwe nisitembee na jeshi la miguu,
Nisipande farasi, nisirushe mizinga;
Huenda kamwe nisiruke juu ya adui,
Lakini mimi niko katika jeshi la Bwana.

³¹⁸ Unaamini unaweza kuimba huo peke yako? Panda hapa juu, kipenzi, njoo papa hapa. Sasa nataka nyote mfanye vile nifanyavyo. Njoni huku, nyuma ya madhabahu hapa, sasa. Njoo huku juu. Kila mmoja wenu, sogeeni papa hapa nilipo, mnaona. Pandeni huku; hakuna mtu anayekaa nje ya madhabahu. Njoni papa hapa juu pamoja nami. Hivyo ndivyo. Vema. Moja kwa moja *hivi*. Sasa geukeni *hivi*, mwangalie kusanyiko hili, namna *hii*. Hivyo ndivyo. Ninataka kuwaonyesha vile wavulana na wasichana wazuri hufanya baada ya kumjua Yesu. Sasa, rudini moja kwa moja hapa, wavulana na wasichana. Sasa ninyi ni . . . Ndivyo hivyo. Sasa angalieni huko nje.

³¹⁹ Sasa ninaposema, “Huenda kamwe nisitembee katika jeshi,” ninyi . . . “nisitembee katika jeshi la miguu,” nanyi mtembee, pia. Ninaposema, “Huenda kamwe nisipande farasi,” mfanye mambo yale yale ninayofanya. Sasa kaeni mbali nami, huko nyuma kabisa sasa, mkitoa nafasi. Nyuma kabisa, nyuma kabisa, sasa mko tayari. Sasa hima, tuimbe. [Ndugu Branham na watoto wanaashiria huku wakiimba—Mh.]

Huenda kamwe nisitembee na askari wa
miguu, (Angalieni!)
Nisipande farasi, nirushe mizinga;
Huenda nisiweze kuruka juu ya adui,
Lakini mimi niko katika jeshi la Bwana.

Loo, mimi niko katika jeshi la Bwana,
Mimi niko katika jeshi la Bwana! (Tayari!)

Huenda nisitembee na jeshi la miguu,
Nisipande farasi, nisirushe mizinga;
Huenda nisiruke juu ya adui,
Lakini niko katika jeshi la Bwana.

³²⁰ Amina! Simameni tu kimya. Ni wangapi wanaoupenda huo? Semeni, “Amina.”

³²¹ Sasa, Baba wa Mbinguni, wabariki watoto hawa wadogo leo. Wao ni Wako, Bwana. Wamekutolea Wewe maisha yao. Wanaisikia hadithi hiyo ndogo ya Musa na jinsi ulivyomlinda. Wanasikia habari za mama mzuri na baba mzuri ambao waliwasaidia na kuwalea. Vivyo hivyo na hawa watoto wadogo wana mama na baba wazuri. Nami naomba, Baba, ya kwamba Wewe utawalinda na kuwaelekeza kwenye mkondo wa wakati, na Malaika wa Mungu wawalinde. Wape . . . Na kisha uwe

kwenye upande wa mapokezi, kuwapokea katika siku za mwisho, Bwana, katika Ufalme Wako. Twaomba katika Jina la Kristo. Amina.

³²² Sasa mnaweza kurudi kwenye viti vyenu na kuwaambia baba na mama jinsi unavyojisikia vizuri. Amina.

³²³ “Siku zote za kuzungukazunguka kwao waliongozwa.” (Mnaujua huo pia?)

...katika mizunguko yao waliongozwa,
Waliongozwa mpaka kwenye nchi ya ahadi;
Kwa mkono wa Bwana katika uongozi wa
hakika,
Waliletwa ukingoni mwa Kanaani.

Kila mtu!

Ishara ya moto usiku,
Na ishara ya wingu mchana,
Ikizunguka-zunguka juu, kabla tu,
Wakisafiri safarini mwetu,
Atakuwa mwelekezi na kiongozi,
Mpaka jangwa lipitwe na wakati,
Kwa kuwa Bwana, Mungu wetu, kwa wakati
Wake mzuri
Atatuongoza kwenye nuru hatimaye.

³²⁴ Ni wangapi walio wagonjwa asubuhi ya leo na wanataka maombi? Hebu tuone mkono wenu. Kwa kuwa tumechelewa kidogo, labda tutaahirisha ibada yetu ya uponyaji hadi usiku wa leo, na tuombe tu dua sasa, maana tumechelewa kidogo.

³²⁵ Je, mumeifurahia hadithi hiyo ndogo? [Kusanyiko linasema, “Amina!”—Mh.] Mnafikiri ilikuwa nzuri kwa watoto wadogo? [“Amina!”] Naam. Sisi—sisi tunawapita mara nyingi. Hatupaswi kufanya hivyo. Mnaona, sipati kamwe nafasi ya kufundisha shule ya Jumapili, na asubuhi ya leo ilikuwa ni wakati wa kuwazungumzia. Sikutaka kuwachosha, lakini nilitaka kuwasimulia hadithi hii ndogo.

³²⁶ Kumbukeni, enyi watoto wadogo, hiyo sio hadithi ndogo ya kale mliyoisoma popote. Hiyo ni ya Kweli. Huo ni Ukweli! Mungu alifanya hivyo. Naye yuko pamoja *nanyi* sasa. Vema.

³²⁷ Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa tunapoimba wimbo wetu wa kufumukana, polepole, “Peleka Jina la Yesu, kama ngao dhidi ya kila adui.” Vema.

Peleka Jina la Yesu,
Mtoto wa huzuni na majonzi.



MAFUNZO JUU YA MUSA SWA56-0513

(Teaching On Moses)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 13 Mei, 1956, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org